BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2018

## 636 TEHAMA

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# UCHAMBUZI WA MAJIBU YA MASWALI YA MITIHANI WA KITAIFA WA DARAJA LA IIIA (GATCE) 2018

## 636 TEHAMA

*Imetolewa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S. L. P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2018**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

**DIBAJI** ........ iv

**1.0 UTANGULIZI** ........ 1

**2.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI** ........ 2

2.1 Swali la 1: Misingi ya Ufundishaji Somo la TEHAMA ........ 2

2.2 Swali la 2: Upimaji ........ 5

2.3 Swali la 3: Ufundishaji wa Mada za Mfano ........ 7

2.4 Swali la 4: Ufundishaji wa Mada za Mfano ........ 10

2.5 Swali la 5: Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la TEHAMA ........ 13

2.6 Swali la 6: Ufundishaji wa Mada za Mfano ........ 16

2.7 Swali la 7: Ufundishaji wa Mada za Mfano ........ 19

2.8 Swali la 8: Ufundishaji wa Mada za Mfano ........ 22

2.9 Swali la 9: Upimaji ........ 25

2.10 Swali la 10: Maandalizi ya Ufundishaji ........ 28

2.11 Swali la 11: Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji Somo la TEHAMA ........ 31

2.12 Swali la 12: Ufundishaji wa Mada za Mfano ........ 36

2.13 Swali la 13: Ufundishaji wa Mada za Mfano ........ 40

2.14 Swali la 14: Upimaji ........ 43

2.15 Swali la 15: Ufundishaji wa Mada za Mfano ........ 48

2.16 Swali la 16: Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la TEHAMA ........ 52

**3.0 UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA KILA MADA** ........ 56

**4.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** ........ 56

4.1 Hitimisho ........ 56

4.2 Mapendekezo ........ 56

**KIAMBATISHO** ........ 58

# DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya Mtihani wa somo la 636 TEHAMA wa kuhitimu Daraja la IIIA (GATCE) Mei 2018, imetayarishwa ili kuwapa mrejesho wadau wa elimu ambao ni wanachuo, wakufunzi, wazazi na watunga sera kuonesha namna watahiniwa walivyojibu maswali pamoja na ufaulu wao. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika taarifa hii umefanyika ili kuonesha maeneo mbalimbali katika muhtasari ambayo watahiniwa walijifunza ipasavyo na yale ambayo hawakujifunza kwa ufasaha.

Mtihani wa Taifa wa Daraja la IIIA (GATCE) ni mtihani wa upimaji tamati unaofanywa na watahiniwa baada ya kuhitimu mafunzo yao kwa muda wa miaka miwili. Lengo la upimaji huu ni kubaini kiwango cha umahiri wao katika matumizi ya TEHAMA waliyoyapata ndani ya kipindi cha miaka miwili ambayo yatatumika kuwafundisha wanafunzi wa shule za msingi Tanzania katika somo la TEHAMA. Aidha, Uchambuzi wa kila swali umefanyika, taarifa zimeoneshwa kwa kutumia majedwali na vielelezo ili kuainisha watahiniwa walioweza kujibu maswali kwa usahihi na wale walioshindwa kujibu kwa usahihi. Pia, taarifa hii imeeleza sababu zilizowafanya baadhi ya watahiniwa kupata alama za juu au chini katika baadhi ya maswali ya mtihani.

Aidha, majibu ya watahiniwa katika mtihani huu yanaashiria kwamba, mfumo wa elimu ulileta au haukuleta ufanisi wa ufundishaji na ujifunzaji katika kipindi cha mafunzo. Uchambuzi huu ulibaini mambo kadhaa ambayo yamechangia kwa baadhi ya watahiniwa kushindwa kujibu maswali ya mtihani kwa usahihi kama vile; kukosa maarifa na ujuzi katika mada husika, ufundishaji wa kinadharia na kutoelewa matakwa ya swali. Baraza la Mitihani la Tanzania linaamini kuwa, taarifa hii ni nyenzo itakayo wasaidia wadau wa Elimu kuchochea utendaji wenye tija katika kujenga mazingira bora ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kutoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani na wadau wengine wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii, pia Baraza litashukuru kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa wadau wa Elimu ili kuboresha taarifa ya uchambuzi wa maswali ya Mtihani wa TEHAMA katika ngazi ya Daraja la IIIA siku za usoni.



Dkt. Charles E. Msonde

**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Uchambuzi wa ripoti hii unaonesha kiwango cha ufaulu wa mtihani wa Taifa wa ualimu katika somo la TEHAMA kwa watahiniwa waliohitimu Mafunzo ya Ualimu Daraja la IIIA (GATCE) mwezi Mei, 2018.

Mtihani huu ulitungwa ili kutathmini umahiri na ujuzi walioupata watahiniwa kwa kuzingatia mwongozo wa utungaji mitihani wa mwaka 2017 na muhtasari wa somo la TEHAMA wa mwaka 2009. Mtihani huu uligawanyika katika sehemu mbili, sehemu A na sehemu B. Sehemu A ilikuwa na maswali 10 yenye alama 4 kwa kila swali ambapo mtahiniwa alitakiwa kutoa maelezo mafupi. Sehemu B ilikuwa na maswali 6 na kila swali lilikuwa na alama 15. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali 4 tu kutoka sehemu hii.

Katika mtihani wa Taifa wa somo la TEHAMA mwaka 2018, jumla ya watahiniwa waliosajiliwa walikuwa 4945 ambapo wasichana walikuwa 1913 na wavulana walikuwa 3032. Jumla ya watahiniwa 4887 walifanya mtihani huo ikiwa ni wasichana 1891 na wavulana 2996. Aidha, watahiniwa 4851 (99.67%) walifaulu mtihani huo. Mchanganuo wa ufaulu kwa maswali na mada zilizotahiniwa umeoneshwa katika **Kiambatisho**.

Aidha, katika uchambuzi wa majibu ya watahiniwa, ufaulu wao uligawanywa katika viwango vitatu ambao ni vizuri, wastani au dhaifu kutokana na asilimia ya watahiniwa waliopata asilimia 40 au zaidi ya alama za swali husika. Hivyo, asilimia 70 hadi 100 ni ufaulu mzuri, 40 hadi 69 ni ufaulu wa wastani na 0 hadi 39 ni ufaulu hafifu. Viwango hivi vilitumika pia kuonesha ufaulu wa mtahiniwa kwa kila mada. Katika uchambuzi wa maswali, chati zenye rangi za kijani, njano na nyekundu zimeambatanishwa kwa kila swali ili kufafanua viwango vya ufaulu wa watahiniwa hao. Rangi ya kijani inawakilisha ufaulu mzuri, rangi ya njano inawakilisha ufaulu wa wastani na rangi nyekundu inawakilisha ufaulu hafifu.

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa umefanyika kwa kuonesha mahitaji ya swali, mgawanyo wa alama, ubora na udhaifu wa majibu ya watahiniwa. Vile vile, sampuli za sehemu ya majibu mazuri na dhaifu kutoka kwa watahiniwa zimeambatanishwa katika kila swali.


## 2.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

Sehemu hii inatoa uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika maswali yote ya sehemu A na B. Katika sehemu A mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote kwa kifupi na sehemu B mtahiniwa alipaswa kuchagua maswali manne na kuyajibu kwa mfumo wa insha. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulifanyika kwa kuzingatia idadi ya watahiniwa waliojibu swali husika kwa usahihi na wale ambao hawakujibu kwa usahihi kulingana na matakwa ya swali.

### 2.1 Swali la 1: Misingi ya Ufundishaji Somo la TEHAMA

Swali hili lilimtaka mtahiniwa afafanue kwa kifupi mambo manne yanayoweza kuhatarisha usalama wa wanafunzi na vifaa vya kujifunzia wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA.

Katika uchambuzi wa swali hili, imeonekana kuwa watahiniwa 4887 sawa na asilimia 100 walifanya ambapo asilimia 58.7 walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5, asilimia 20.9 walipata kuanzia alama 2.0 hadi 2.5 na asilimia 20.4 walipata alama 3.0 hadi 4.0. Kwa ujumla ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani asilimia 41.3 walipata zaidi ya alama 1.5 kama ilivyooneshwa kwenye Kielelezo Na.1.





**Kielelezo Na. 1:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1*

Watahiniwa waliojibu swali hili kwa usahihi, ambao ni asilimia 41.3 waliweza kufafanua mambo manne yanayoweza kuhatarisha usalama wa wanafunzi na vifaa vya kujifunzia wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA. Kwa mfano, mtahiniwa mmojawapo aliandika majibu yafuatayo: “(i) Kuchubuka kwa nyaya za umeme (ii) Vumbi (iii) Mwanga

hafifu na (iv) Unyevunyevu/maji darasani”. Kielelezo Na. 1.2 ni sampuli ya jibu sahihi la mmoja kati ya watahiniwa waliojibu vizuri swali hili.

**Kielelezo Na. 1.2**



use only

1. Kufafanua mambo manne ambayo yanaweza kuhatarisha usalama wa mwanafunzi na vifaa vya kujifunzia wakati wa kufundisha somo la TEHAMA.

i/ Kuwepo na nyaya zilizochubuka, kama mwalimu anafundisha kwa kutumia kompyuta ni kama kutakuwa na nyaya zilizo chubuka basi ni rahisi kusababisha hatari kwa mwanafunzi

ii/ unyevu nyevu, katika kutumia vifaa vya TEHAMA kama kuna unyevunyevu sehemu ulipoweka chombo husika cha kufundishia kwa mfano radio, magazeti ni rahisi kuharibika na kuweza kukosa kufanya kazi

iii/ Mwanga hafifu, wakati mwingine unakuta madarasa hayana mwanga wa kutosha kitu ambacho kinaweza kusababisha uoni hafifu kwa wanafunzi au kuwa na tatizo la kutokuona kabisa.

iv/ Kuwepo kwa vumbi darasani, katika shule zetu hasa za serikali na shule za msingi madarasa mengi yanakuwa na vumbi kutoka na sakafu kubomoka au kutokuwepo kabisa hasa vijijini kitu ambacho kinaweza kupelekea mtoto kuwa na tatizo la kifua kila mara kutokana na vumbi pia kama kuna vyombo unatumia vya TEHAMA ni rahisi kujaa vumbi na kupelekea kuharibika kutofanya kazi kabisa.

Katika Kielelezo Na.1.3 mtahiniwa alifafanua kwa usahihi mambo manne yanayoweza kuhatarisha usalama wa wanafunzi na vifaa vya kujifunzia wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA kulingana na matakwa ya swali.

Katika swali hili, asilimia 58.7 walishindwa kufafanua mambo manne yanayoweza kuhatarisha usalama wa wanafunzi na vifaa vya kujifunzia wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA. Hii inaonesha kuwa watahiniwa hawa walikosa maarifa kuhusu *Misingi ya Ufundishaji Wa Somo la TEHAMA.mada za mfano,* mtahiniwa mmoja aliandika,

(i) Uwepo wa vihatarishi kama nyuki darasani wanaweza kukung’ata
(ii) Uwepo wa vurugu na kelele darasani
(iii) Miundo mbinu mibovu,kama majengo yamechoka yanawezakuanguka na kujeruhi watoto.
(iv) Matumizi ya zana hatarishi kama vile bunduki na sumu.


Aidha mtahiniwa mwingine alijikita kufafanua mambo manne ya jumla yanayo weza kuathiri ufundishaji kwa ujumla badala ya kujikita kwenye ufafanuzi wa mambo yanayo weza kuhatarisha usalama wa wanafunzi na vifaa. Mtahiniwa huyo aliandika majibu yake kama ifuatavyo:

(i) Kutumia zana ambazo ni hatarishi mfano kisu na anaweza kujikata.
(ii) Kutumia zana ambazo hazijafanyiwa majaribio kujua kama ni salama au si salama.
(iii) Mwalimu kutumia zana ambazo wanachuo hawana ujuzi nazo mfano matumizi au jinsi ya kutumia umeme.
(iv) Mwalimu kuandaa zana ambazo hazilingani na umri na uelewa wa wanafunzi.

Mtahiniwa mwingine alifafanua kuhusu kukosekana kwa usikivu, msongo wa mawazo na athari za kimaumbile badala ya kuelezea vihatarisha vya usalama wa mwanafunzi na vifaa vyake katika muktadha wa TEHAMA ambavyo ni unyevunyevu au maji, ukosefu wa hewa yakutosha, kuchubuka kwa nyaya za umeme, vumbi na mpangilio mbaya wa darasa.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa waliofanya vibaya unaonesha kuwa baadhi yao walihawilisha maarifa ya somo jingine. Kwa mfano baadhi ya watahiniwa walihawilisha maarifa ya somo la Mtaala wa elimu na ufundishaji na kuingiza katika somo la TEHAMA bila kuangalia muktadha wa swali na mazingira yake. Kielelezo Na. 1.3 kinaonesha mtahiniwa aliyeshindwa kufanunua kwa kifupi mambo manne yanayoweza kuhatarisha usalama wa wanafunzi na vifaa vya kujifunzia wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA.

**Kielelezo Na.1.3**



1. i) Vurugu darasani - hii hutokea endapo darasa halitakuwa katika hali ya utulivu.

ii) Mwalimu kutumia zana hatari katika ufundishaji na kumtaka kila mwanafunzi ajijaribishe.

iii) Matumizi ya kemikali kama zana - hii huweza kupelekea wanafunzi kumwagiana kemikali endapo hawatakuwa waangalifu katika kutumia.


iv) Ugomvi darasani - Ugomvi kati ya wanafunzi huweza kuhatarisha usalama wao.

Katika Kielelezo Na. 1.3 mtahiniwa aliandika mambo yanayoweza kuathiri ufundishaji kwa ujumla bila kuangalia muktadha wa TEHAMA ambayo ni vurugu darasani, matumizi ya zana hatarishi na ugomvi.

## 2.2 Swali la 2: Upimaji

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa kifupi mambo manne muhimu ya kuzingatia katika utunzi wa maswali ya kuchagua jibu sahihi katika somo la TEHAMA.

Kutokana na uchambuzi uliofanyika katika swali hili, jumla ya watahiniwa 4887 walilifanya ambapo asilimia 67.3 walipata alama 0 hadi 1.5, asilimia 26.5 walipata alama 2 hadi 2.5 na wachache sana ambao ni asilimia 6.2 walipata alama 3 hadi 4. Hivyo, uchambuzi huu umebaini kuwa swali hili limefanyika vibaya kwani ni watahiniwa wachache tu (32.7%) ndio waliopata alama 2 hadi 4 kama ilivyooneshwa kwenye Kielelezo Na. 2.1.




**Kielelezo Na. 2.1:** *Ufaulu wa Watahiniwa Swali la 2*

Watahiniwa walio wengi (67.3%) walishindwa kueleza kwa kifupi mambo manne muhimu ya kuzingatia katika utunzi wa maswali ya kuchagua jibu sahihi katika somo la TEHAMA. Kutokana na uchambuzi wa majibu haya imedhihirika kwamba watahiniwa walio wengi hawana maarifa ya kutosha kuhusu mambo ya kuzingatia wakati wa kutunga maswali ya kuchagua kwa ujumla. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika;


(i) Uzingatiaji wa idadi ya maswali: Katika utunzi huu ni lazima kuzingatia idadi ya maswali.
(ii) Uzingatiaji wa utoaji wa alama kulingana na idadi ya maswali uliyotoa.
(iii) Uzingatiaji wa muda:Ni muhimu kuzingatia muda.
(iv) Kuandaa mwongozo wa usahihishaji: Mwalimu unatakiwa kuandaa mwongozo wa usahihishaji wakati wa kutoa alama kwa wanafunzi.

Pia mtahiniwa mwingine aliyekosa swali hili alijibu kama ifuatavyo:

(i) kuchagua mada husika.
(ii) kuchagua Mada ndogo kutoka mada husika.
(iii) kuchagua swali lenye majibu tofauti tofauti.
(iv) kuandika swali hilo na majibu yake katika vipengele tofauti tofauti.

Majibu haya yanaonesha kuwa watahiniwa walikosa maarifa kuhusu mambo muhimu ya kuzingatia katika utunzi wa maswali ya kuchagua jibu sahihi katika somo la TEHAMA. Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi la mmoja kati ya watahiniwa waliojibu vibaya swali hili.

**Kielelezo Na 2.2**


2: i) Wazo kuu
ii) Namna ya maneno au neno
iii) kuwa na maarifa ya swali kuhusiana na maswali hayo
iv) kufahamu mada ya maswali hayo kwa kina


Katika Kielelezo Na 2.2 mtahiniwa alitaja mambo ya kuzingatia wakati wa kutunga mtihani kwa ujumla badala ya kuandika majibu sahihi ambayo ni; Jibu sahihi kuwa moja, maudhui na machaguo, sentensi rahisi, maelezo yanayo eleweka na idadi sawa ya machaguo.

Watahiniwa waliojibu swali hili kwa usahihi waliweza kueleza kwa kifupi mambo manne muhimu ya kuzingatia katika utunzi wa maswali ya kuchagua jibu sahihi katika somo la TEHAMA. Kwa mfano, mtahiniwa mmojawapo alijibu kama ifuatavyo:

(i) Upande wa majibu, jibu moja liwe sahihi na vingine viwe vichachawizi.
(ii) Nafasi ya majibu sahihi ibadilike kwa kila swali.
(iii) Majibu yawe na maana inayoelekeana.
(iv) Maswali yenye ukanushi yasitungwe.

Majibu haya yanadhihirisha kuwa watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya utunzi wa maswali ya kuchagua. Kielelezo Na. 2.3 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo Na. 2.3**



2. Mambo ya kuzingatia wakati wa utunzi wa maswali ya kuchagua jibu sahihi
(i) Hakikisha swali linakuwa na vichachawizi vinne au vitano mfano A, B, C, D na E.
(ii) Hakikisha kunakuwa na jibu sahihi moja tu kwa kila swali
(iii) Hakikisha herufi ya jibu inabadilika kwa kila swali. mfano kama swali la kwanza likawa jibu B swali la pili iwe herufi nyingine
(iv) Hakikisha urefu wa sentensi unafanana ili kuto mchanganya mwanafunzi

Katika Kielelezo Na. 2.3 mtahiniwa aliweza kueleza kwa usahihi mambo manne yanayotakiwa kuzingatiwa wakati wa kutunga maswali ya kuchagua, ambayo ni,swali kuwa na vichachawizi vinne, kuwepo na jibu sahihi moja, kubadilika kwa nafasi ya jibu kwa kila swali na urefu wa sentensi.

## 2.3 Swali la 3: Ufundishaji wa Mada za Mfano

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kubainisha vifaa vinne na namna vinavyoweza kutumika kufundishia mada ya kuelezea kwa usahihi habari iliyosemwa.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili umebainisha kwamba, kati ya watahiniwa 4887 asilimia 21.6 walipata alama 0 hadi 1.5, asilimia 46.2 walipata alama 2 hadi 2.5 na asilimia 32.2 walipata alama 3 hadi 4. Hivyo, kwa matokeo haya ya uchambuzi watahiniwa walio wengi (78.4%) walifanya vizuri kwani walipata alama 2 hadi 4, kama ilivyooneshwa katika Kielelezo Na. 3.1.




**Kielelezo Na. 3.1:** *Ufaulu wa Watahiniwa Swali la 3*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, asilimia 78.4 waliweza kubainisha kwa usahihi vifaa vinne na namna vinavyoweza kutumika kufundishia mada ya kuelezea kwa usahihi habari iliyosemwa. Hii inaonesha kuwa watahiniwa hawa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu *Ufundishaji wa Mada za Mfano*. Yafuatayo ni baadhi ya majibu sahihi ya watahiniwa waliofanya vizuri katika swali la 3 kama yaliyopatikana kwenye vijitabu vyao vya kujibia:

(i) Redio: Unaweza kutumia redio kwa wanafunzi kusikiliza kisha kueleza jambo lililosemwa kwenye redio kwa usahihi.

(ii) Televisheni: Mwalimu anaweza kuwaambia wanafunzi watazame na kusikiliza televisheni kwa makini kisha kueleza habari iliyosemwa.


(iii) Simu: Mwalimu anaweza kutumia simu kwa wanafunzi wasikilize habari fulani kisha waeleze habari waliyosikiliza au iliyosemwa.

(iv) Kompyuta: Mwalimu anaweza kueleza wanafunzi kwa kutumia sauti iliyo hifadhiwa kwenye kompyuta kisha wanafunzi waeleze habari iliyosemwa kwa usahihi.

Zaidi ya hayo majibu, mtahiniwa mwingine aliweza kubainisha kwa kutaja vifaa hivyo na kuvielezea namna vitakavyotumika katika ufundishaji wa

mada hiyo ambavyo ni redio, runinga, simu ya mkononi na kitarakirishi. Mtahiniwa huyo alifafanua kwamba kila mwisho wa kusikiliza maswali yatafuata ili kupima kama waliweza kusikiliza. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa atika swali la 3 umeonesha pia kwamba wapo watahiniwa waliweza kubainisha kwa usahihi vifaa vine kama tape rekoda, kanda,magazeti na simu na kuelezea namna vinavyoweza kutumika kufundishia mada ya kuelezea kwa usahihi habari iliyosemwa. Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya mtahiniwa aliyeweza kubainisha vifaa hivyo na namna vinavyoweza kutumika kufundishia mada ya kuelezea kwa usahihi habari iliyosemwa.

**Kielelezo Na. 3.2**



| 3. | VIFAA | NJINSI VINAVYOTUMIKA. |
|---|---|---|
| | i) Tape rekoda | - Kurekodi na kusikiliza tena habari. |
| | ii) Kanda. | - Kusikiliza kupitia redio kaseti |
| | iii) Magazeti | - Kusoma kwa ufasaha na usahihi. |
| | iv) Simu | - Kurekodi na kusikiliza kwa usahihi |

Kielelezo Na. 3.2 Kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliweza kubainisha vifaa vinne ambavyo ni; Tape rekoda, Kanda, Magazeti na simu.

Pamoja na kwamba watahiniwa walio wengi waliweza kujibu swali hili vizuri, kuna watahiniwa wachache ambao hawakuweza kujibu vizuri, kwa mfano mtahiniwa mmojawapo aliandika;


(i) Muhtasari.
(ii) Kitabu cha kiada.
(iii) Kiongozi cha mwalimu.
(iv) Maandiko ya rejea.

Mtahiniwa mwingine katika kujibu swali hili aliandika;

(i) Daftari.
(ii) Andalio la somo.
(iii) Muhtasari.
(iv) Kiongozi cha mwalimu.

Majibu haya yanaashiria kuwa watahiniwa walikosa maarifa ya kubainisha vifaa vinne na namna vinavyoweza kutumika kufundishia mada ya kuelezea kwa usahihi habari iliyosemwa. Kielelezo Na. 3.3 kinaonesha mfano wa jibu lisilo sahihi toka kwa mtahiniwa aliyeshindwa kubainisha vifaa vinne na namna vinavyoweza kutumika kufundishia mada ya kuelezea kwa usahihi habari iliyosemwa.

**Kielelezo Na. 3.3**


3 Vifaa vinavyoweza kufumika kufundishia mada ya kuelezea kwa usahihi habari iliyosemwa.
i. Nyimbo
ii. hadithi
iii. Majibizano
iv. Dialojia .


Kielelezo Na. 3.3 Kinaonesha kuwa mtahiniwa aliandika mbinu kama vile; nyimbo, hadithi, majibizano na dialojia badala ya kuandika Redio, Television, Simu ya mkononi na machapisho.

## 2.4 Swali la 4: Ufundishaji wa Mada za Mfano

Katika swali hili, mtahiniwa alitakiwa kutoa tofauti nne kati ya magazeti na majarida.

Uchambuzi wa jumla uliofanyika katika swali hili ulionesha kuwa, kati ya watahiniwa 4887, asilimia 91.9 walipata alama 3 hadi 4, asilimia 4.7 walipata alama 2 hadi 2.5 na asilimia 3.4 walipata alama 0 hadi 1.5. Hii inaonesha kuwa swali hili lilijibiwa vizuri kwani asilimia 96.6 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 2 hadi 4, kama ilivyooneshwa katika

**Kielelezo Na. 4.1.**





**Kielelezo Na 4.1***: Ufaulu wa Watahiniwa Swali la 4*

Aidha, uchunguzi zaidi umeonesha kuwa waliopata alama 2 hadi 4 walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya magazeti na majarida. Uchunguzi huu unaonesha kuwa watahiniwa wengi walilielewa swali na kujibu vizuri kulingana na matakwa ya swali. Majibu sahihi ya baadhi ya watahiwa yaliyopatikana kwenye vijitabu vyao vya kujibia ni kama yafuatayo:

| **Magazeti** | **Majarida** |
|---|---|
| (i) Hutolewa na kuchapishwa kila siku. | Hutolewa kila baada ya wiki, mwezi au mwaka. |
| (ii) Hutoa habari kuhusu mambo mbalimbali. | Hujikita katika swala moja mfano jarida linalo husu masuala ya ugonjwa wa UKIMWI. |
| (iii) Hayana gharama kubwa. | Yana gharama kubwa. |
| (iv) Taarifa zake huweza kubadilika kila siku. | Taarifa zake haziwezi kubadilika kila siku. |

Pia, Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha mfano wa jibu sahihi kutoka kwa mtahiniwa aliyeweza kutofautisha kati ya Majarida na Magazeti.

**Kielelezo Na. 4.2**



4. Tofauti 4 ailiozopo kati ya Magazeti na Majarida.

| MAGAZETI | MAJARIDA. |
|---|---|
| i/ Huandikwa na mtu yeyote yule au mwandishi yeyote. | i/ Huandikwa na Wataalamu baada ya kufanya utafiti. |
| ii/ Hueleza habari mbali mbali kama vile michezo burudani siasa, utamaduni afya. | ii/ Hueleza mada au habari moja tu kwa kina na kwa undani. |
| iii/ Habari huwahusu makundi yote katika jamii kama vile vijana, watoto watu wa makamo na wazee. | iii/ Habari huwahusu kundi moja tu katika jamii. Kama vile Fema huwa lenga sana Vijana |
| iv/ Hueleza matukio au habari hutolewa kila siku | iv/ Habari hutolewa kwa muda mrefu kama vile wiki, mwezi na zaidi. |

Katika Kielelezo Na. 4.1, mtahiniwa aliweza kutofautisha kati ya Majarida na Magazeti kwa kuonesha wahusika katika uandaaji, aina ya maudhui na muda wa upatikanaji.

Hata hivyo, watahiniwa wachache hawakujibu kwa usahihi kwa kadri ya matakwa ya swali. Watahiniwa hawa walionekana kutokuwa na umahiri wa kutosha juu ya tofauti iliyopo kati ya magazeti na majarida. Changamoto hii inaweza kuwa imesababishwa na kukua kwa utandawazi ambapo taarifa nyingi hupatikana kwenye mitandao. Baadhi ya majibu ya watahiniwa yasiyo sahihi katika swali hili ni haya yafuatayo:

| **Magazeti** | | **Majarida** |
|---|---|---|
| (i) | Hutumika katika kuelimisha jamii. | Hayaelimishi jamii. |
| (ii) | Huandikwa kwa aya. | Hayana aya. |
| (iii) | Hueleza matukio yaliyotokea. | Hayaelezi matukio mbalimbali. |
| (iv) | Ni chanzo cha taarifa. | Siyo chanzo cha taarifa. |

Vile vile, mtahiniwa mwingine aliandika jibu lisilo sahihi katika swali hili kama ifuatavyo:

(i) Magazeti hutoa taarifa kamili lakini majarida hutoa au huonesha utangulizi au kichwa cha habari.
(ii) Magazeti hutoa picha ya maneno lakini majarida hutoa ujumbe wa maneno tu.
(iii) Magazeti huonesha wahariri majarida hayaoneshi wahariri bali hutaja makampuni yao.

Pia, mtahiniwa mwingine alijibu kuwa tofauti ya magazeti na majarida ni kwamba;

**Magazeti:**


(i) Hutoa elimu kwa wasomaji (jamii).
(ii) Husaidia kutoa habari ya jambo fulani kwa jamii.
(iii) Hutoa ajira.

**Majarida:**

(i) Huongeza maarifa kwa wasomaji.
(ii) Huongeza maarifa ya kiuchumi.

Kwa ujumla majibu haya yanaonesha kuwa watahiniwa hawana maarifa ya kutosha juu ya tofauti iliyopo kati ya Magazeti na Majarida. Kielelezo Na. 4.3 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutofautisha kati ya Majarida na Magazeti.

**Kielelezo Na. 4.3**




| 4. | MAGAZETI | MATARADA. |
|---|---|---|
| | i) Ni kama makaratasi ~~meupa~~ meupe | i) Ni kama ~~vitabu~~ makaratasi ya rangi ya tunde. |
| | ii) Yana maandishi | ii) Hayana maandishi. |
| | iii) Ni gharama | iii) Sio gharama. |
| | iv) Yana jina la kampuni | iv) Hayana jina la kampuni. |

Katika Kielelezo Na. 4.3, mtahiniwa aliandika tofauti juu ya rangi za karatasi, aina ya maandishi, gharama na kampuni, badala ya aina ya ujumbe, muda, namba ya utambulisho (ISSN) na bei zake.

## 2.5 Swali la 5: Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la TEHAMA

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kuainisha vifaa vinne anavyohitaji mwalimu wa somo la TEHAMA katika kuandaa azimio la kazi.

Watahiniwa 4887 walifanya swali hili; uchambuzi uliofanyika katika swali hili umeonesha kuwa, asilimia 46.1 walipata alama 0 hadi 1.5, asilimia 45.2 walipata alama 2 hadi 2.5 na asilimia 8.7 walipata alama 3 hadi 4. Katika swali hili, watahiniwa walifaulu kwa kiwango cha wastani kwani asilimia 53.9 walipata zaidi ya alama 1.5, kama inavyoonesha katika Kielelezo Na. 5.1.




**Kielelezo Na. 5.1:** *Ufaulu wa Watahiniwa Swali la 5*


Baada ya kufanya uchunguzi yakinifu imebainika kwamba watahiniwa wengi (53.9%) walikuwa na uelewa mzuri kuhusu vifaa vinavyohitajika wakati wa kuandaa azimio la kazi. Hii imetokanana ukweli kwamba mada hiyo hufundishwa kwenye masomo mengine hivyo watahiniwa walipata fursa ya kuhawilisha maarifa.

Majibu sahihi ya baadhi ya watahiniwa yaliyopatikana kwenye vijitabu vyao vya kujibia yanadhihirisha ufaulu huu kama ifuatavyo:

(i) Muhtasari wa somo.
(ii) Kalenda ya mwaka.
(iii) Kalenda ya shule.
(iv) Kitabu cha kiada.


Kielelezo Na. 5.3 ni sampuli ya mtahiniwa aliyeweza kuainisha vifaa vinne anavyohitaji mwalimu wa somo la TEHAMA katika kuandaa azimio la kazi.

**Kielelezo Na. 5.3**



Qn 5 Vifaa vinne vya kuandaa Azimio la kazi ni

i) Muhtasari: Ni kifupisho cha maandhi yote yaliyopangwa kufundishwa kulingana na ngazi husika ya Elimu na darasa husika, Huu huwa na maelekezo muhimu katika uandaaji wa Azimio kwani huwa na Mada, Malengo makuu na malengo mahsusi, muda utakaotumika (idadi ya vipindi), Pia zana, nk


ii) Kiongozi cha Mwalimu, Hiki ni Kitabu Ambacho humwongoza Katika ufundishaji wake Mfano Mbinu na njia za Kufundishia zana au Mfano vya Kufundishia na Kujifunzia n.k.

iii) Kalenda ya Shule, Hii ni Kalenda ambayo huonyesha Matukio yatakayofanyika Shuleni hapo Mfano Mitihani, Majaribio, Mashindano Mbalimbali ya Kimichezo n.k.

iv) Kalenda ya Mwaka, Hii Pia ni Kalenda Ambayo huonyesha Matukio yanayotendeka Kwa Kila Nchi nzima Mfano Sherehe Mbalimbali za Nchi Mfano Sherehe za Muungano, Sherehe za wakulima na Wafanyakazi (Mei mosi), Sherehe za Mwaka Mpya n.k.

Kielelezo Na. 5.1: kimeonesha mtahiniwa aliyeweza kuainisha vitu vyote vya msingi pamoja na kuvifafanua kama vile: muhtasari, kiongozi cha mwalimu, kalenda ya shule na kalenda ya mwaka.

Kwa upande mwingine, uchanganuzi huu unaonesha kwamba watahiniwa (46.1%) hawakufanya vizuri swali hili kwani walipata alama 0 hadi 1.5. Hii inaonesha kuwa watahiniwa hawa hawana umahiri wakubainisha vifaa hivyo, ama walishindwa kutafsiri kiini cha swali kama ambavyo baadhi ya majibu ya baadhi ya watahiniwa ambao hawakujibu kwa kadri ya matakwa ya swali yanavyoonesha. Mtahiniwa mmojawapo katika kulijibu swali hili aliandika kama ifuatavyo:

(i) Andalio la somo.
(ii) Muhtasari.
(iii) Kiongozi cha mwalimu.
(iv) Shajala la somo.


Mtahiniwa mwingine katika kujibu swali hili aliandika kama ifuatavyo:

(i) Zana za kufundishia.
(ii) Kitabu cha ziada.
(iii) Andalio la somo.
(iv) Rejea mbalimbali.

Sambamba na hayo, watahiniwa wengi (45.2%) waliweza kuainisha kwa usahihi vifaa viwili na vingine walikosa jambo ambalo liliwafanya watahiniwa hao kupata alama 2 hadi 2.5. Uchambuzi unaonesha kwamba

watahiniwa hawakuelewa matakwa ya swali na maana ya neon, "ainisha" kwani walitaja tu. Kielelezo Na. 5.2 ni sampuli ya mtahiniwa aliyeshindwa kuainisha vifaa vinne anavyohitaji mwalimu wa somo la TEHAMA katika kuandaa azimio la kazi.

**Kielelezo Na. 5.2**



05· i/ Muhtasari·
ii/ Daftari au karatasi·
iii/ Kalamu ya wino na penseli·
iv/ Rula ya kupigia mstari·

Katika Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kubainisha vifaa vinavyohitajika wakati wa kuandaa azimio. Mtahiniwa huyo aliandika; daftari, kalamu na rula badala ya kalenda, muhtasari, kitabu cha kiada na kiongozi cha mwalimu na ratiba ya shule.

## 2.6 Swali la 6: Ufundishaji wa Mada za Mfano

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kubainisha matatizo manne yanayowakumba wakutubi katika kazi yao ndani ya Maktaba.

Katika uchambuzi wa swali hili imebainika kuwa; watahiniwa 4887 walifanya swali hili. Asilimia 61.5 walipata alama 3 hadi 4, asilimia 29.6 walipata 2 hadi 2.5 na asilimia 8.9 walipata alama 0 hadi1.5. Hivyo, kwa matokeo haya ufaulu wa jumla ulikuwa mzuri kwa asilimia 91.1, kama kinavyoonesha Kielelezo Na.6.1.





**Kielelezo Na. 6.1:** *Ufaulu wa Watahiniwa Swali la 6*

Uchambuzi uliofanyika katika swali hili unaonesha kwaba watahiniwa waliofanya vizuri (91.1%) walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu matatizo yanayowakumba wakutubi katika kazi yao ndani ya Maktaba. Yafutayo ni majibu sahihi ya baadhi ya watahiniwa yaliyopatikana kwenye vijitabu vyao vya kujibia:

- (i) Kupotea kwa baadhi ya machapisho ya vitabu, endapo usimamizi hautakuwa makini.
- (ii) Uhaba wa vitabu vya kujisomea kwa wanafunzi na jamii: Haya ni matatizo ambayo wanakumbana nayo wakutubi.
- (iii) Uharifu na wizi wa vitabu: Wapo wanajamii wanapokuwa katika maktaba wanaondoka na vitabu.
- (iv) Mpangilio mbaya wa vitabu: Watumiaji wanapotoka maktaba huwa wanaacha vitabu ovyo.

Vile vile, mtahiniwa mwingine aliandika kuhusu kuibiwa kwa baadhi ya vitabu, uhaba wa vitabu, hali inayopelekea mkutubi kushindwa kutoa huduma hiyo kwa ufanisi na uhaba au kutokuwepo kwa vifaa vya kumsaidia Mkutubi kufanya kazi yake kwa ufanisi kama vile katalogi ya kuongozea uazimaji wa vitabu. Kielelezo Na. 6.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kubainisha kwa usahihi matatizo manne yanayowakumba Wakutubi katika kazi yao ndani ya Maktaba.

**Kielelezo Na. 6.2**


6. Changamoto au matatizo yanayowakumba wakutubi wanapokuwa katika kazi yao katika maktaba ni:
(i) Watumiaji wa maktaba kutokufuata sheria na kanuni za maktaba.
(ii) Kupotea kwa vitabu mbalimbali maktaba (wizi).
(iii) Watu kupiga kelele maktaba.
(iv) Watumiaji wa maktaba kutokurudisha vifaa au vitabu maktaba kwa muda muafaka.

Katika Kielelezo Na. 6.2 mtahiniwa aliweza kujibu swali kwa usahihi ambapo aliandika juu ya kutofuata sheria, upotevu wa vitabu na kutorejesha vitabu kwa wakati.

Kwa upande mwingine, wapo watahiniwa wachache (8.9%) ambao hawakuweza kujibu vizuri swali hili. Sababu zaweza kuwa ni kutofundishwa au kwenye vyuo vyao kutokuwepo na Maktaba. Majibu ya watahiniwa hawa yanaonesha kuwa wanaufahamu kuhusu kazi za Mkutubi na matatizo anayoweza kukumbana nayo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijibu kama ifuatavyo:


(i) Ukosefu wa utaalamu wa kazi yao.
(ii) Upungufu wa vitabu.
(iii) Lugha inayotumika katika vitabu.
(iv) Maktaba kuwa ndogo.

Aidha mtahiniwa mwingine aliandika majibu yafuatayo:

(i) Hitalafu ya umeme na kusababisha kuunguza vitabu.
(ii) kuharibika kwa mfumo wa maji.
(iii) milipuko ya gesi.

Zaidi ya hayo, watahiniwa wengine waliandika kuhusu mishahara midogo, chamangamoto za kuwasiliana na wageni toka nje, ukosefu wa semina, kashfa na matumizi mabaya ya lugha, magonjwa kutokana na hali ya hewa ya Maktaba. Majibu ya watahiniwa hawa yanadhihirisha kuwa walikosa maarifa juu *Ufundishaji wa Mada za Mfano*. Kielelezo Na. 6.3 ni mfano wa majibu yasiyo sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa.

**Kielelezo Na. 6.3**





Katika kielelezo Na. 6.3 mtahiniwa ametaja ajali, migogoro na wizi, badala ya kubainisha juu ya kufanya kazi ya kuelimisha wasiojua matumizi ya Maktaba, watumiaji kutokuwa na maadili mazuri, kutozingatia sheria na uchakavu wa rafu.

## 2.7 Swali la 7: Ufundishaji wa Mada za Mfano

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kuchanganua tofauti nne kati ya barua ya kawaida na barua ya rejesta.

Katika uchambuzi wa ufaulu ilibainika kuwa watahiniwa 4885 walifanya swali hilli na watahiniwa 2 hawakufanya. Aidha, asilimia 45.4 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 1.5, asilimia 40.2 walipata alama 2 hadi 2.5 na asilimia 14.4 walipata alama 3 hadi 4, kama Kielelezo Na. 7.1 kinavyoonesha. Kwa ujumla ufaulu wa swali hili ulikuwa katika kiwango cha wastani kwani asilimia 54.6 walipata alama zaidi ya 1.5.




**Kielelezo Na. 7.1:** *Ufaulu wa Watahiniwa Swali la 7*

Aidha, uchambuzi uliofanyika katika swali hili umeonesha kuwa watahiniwa waliofanya vizuri ni asilimia 54.6. Majibu ya watahiniwa yanaonesha kuwa walikuwa na ufahamu mzuri juu ya barua na rejesta.Yafutayo ni majibu sahihi ya baadhi ya watahiniwa kama yaliyopatikana kwenye vijitabu vyao vya kujibia:

| **Barua ya kawaida** | **Barua ya rejesta** |
|---|---|
| (i) Haina njia maalum ya kutuma. | Ina njia maalum ya kutuma. |
| (ii) Ni rahisi kupotea. | Si rahisi kupotea. |
| (iii) Huchelewa kufika sehemu husika. | Hufika kwa wakati. |
| (iv) Ina gharama kidogo. | Ni gharama kubwa. |

Mtahiniwa mwingine aliandika kama ifuatavyo:

| **Barua ya kawaida** | | **Barua ya rejesta** |
|---|---|---|
| (i) | Bahasha ni ya kawaida. | Bahasha ni maalum. |
| (ii) | Haina gharama kubwa. | Ina gharama kubwa. |
| (iii) | Inatumwa kwa utaratibu wa kawaida. | Inatumwa kwa utaratibu maalu. |
| (iv) | Ni rahisi kuiandaa. | Ni ngumu kuiandaa. |

Majibu ya watahiniwa hawa yanaonesha kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya *Ufundishaji wa Mada za Mfano*. Kielelezo Na. 7.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kutofautisha kati ya barua ya kawaida na rejista.

**Kielelezo Na. 7.2**

7. i) Barua ya kawaida huwekwa katika bahasha ya kawaida lakini barua ya rejesta huwekwa kwenye bahasha maalumu.

ii) Gharama za utumaji wa barua ya kawaida ni ndogo kuliko gharama za utumaji wa barua ya rejesta

iii) Barua ya kawaida huchukua muda mwingi kumfikia mlengwa lakini barua ya rejesta humfikia mlengwa haraka

iv) Barua ya kawaida hupelekwa moja kwa moja katika Sanduku la posta lakini barua ya rejesta hupelekwa kwa mhusika kwa kutumia gari maalumu.

Katika Kielelezo Na. 7.2 mtahiniwa aliandika kuhusu namna ya ufungaji wa bahasha katika pande zote mbili, gharama za utumaji, muda wa kumfikia mtumiwa pia na namna ya upokeaji kwa pande zote mbili, kufuatana na matakwa ya swali.

Pamoja na kwamba watahiniwa waliowengi waliweza kujibu swali hili vizuri, kuna watahiniwa wachache (45.4%) waliopata alama 0 hadi 1.5. Watahiniwa hawa hawakuweza kuchanganua tofauti nne kati ya barua ya kawaida na barua ya rejesta kwa usahihi kwa kadri ya matakwa ya swali, pia baadhi ya watahiniwa waliandika kuhusu barua ya kikazi ambapo haikuwa sehemu ya swali. Majibu ya watahiniwa hawa yanaonesha kuwa baadhi yao walishindwa kutofautisha barua ya kikazi, barua ya kawaida na rejesta. Kwa mfano mtahiniwa mmojawapo aliandika kama ifuatavyo:

| **Barua ya kawaida** | **Barua ya rejesta** |
|---|---|
| (i) Hutumika kwa mawasiliano ya kawaida. | Hutumika kujeshesha jambo. |
| (ii) Hutumia anwani moja. | Hutumia anwani zaidi ya moja. |
| (iii) Huwa ya urafiki. | Huwa ya kikazi. |
| (iv) Huwa na salaam. | Huwa haina salaam. |

Mtahiniwa mwingine alijibu kama ifuatavyo:

| **Barua ya kawaida** | **Barua ya rejesta** |
|---|---|
| (i) Ina anwani moja. | Hii barua ina anwani mbili. |
| (ii) Barua hii ni ya kirafiki. | Barua hii ni ya kikazi. |
| (iii) Ina mambo matano ya kuzingatia. | Ina mambo saba ya kuzingatia. |
| (iv) Haina kichwa cha habari. | Ina kichwa cha habari. |


Aidha, mtahiniwa mwingine aliandika jibu lisilo sahihi kama fuatavyo:

(i) Barua ya kawaida huwa na anwani moja tu lakini barua ya rejista ina anwani mbili.
(ii) Barua ya kawaida haina kichwa cha habari lakini barua ya rejesta ina kichwa cha barua.
(iii) Barua ya kawaida ina maelezo mengi lakini rejista haina maelezo mengi.
(iv) Barua ya kawaida mwandishi haina jina au cheo cha mwandishi lakini barua ya rejista ina cheo cha mwandishi.

Kwa ujumla watahiniwa waliofanya vibaya katika swali hili walikuwa na majibu msambazo sana kama vile; barua ya kawaida hutumwa kwa maandishi na rejista kutumwa kwa maandishi na picha, katika utumaji

baadhi ya watahiniwa waliandika kuwa barua hutumwa kwa njia ya posta na rejista hutumwa kwa mtandao. Majibu haya yanaonesha kuwa watahiniwa hawa hawana maarifa ya kuchanganua tofauti kati ya barua ya kawaida na barua ya rejesta. Kielelezo Na. 7.3 ni sampuli ya majibu kutoka kwa mmoja wa mtahiniwa waliyeshindwa kujibu swali hili.

**Kielelezo Na. 7.3**



7 Barua za kawaida, huandikwa kwa lengo maalumu kwa mfano kusalimiana, kutoa taarifa, kuomba ruhusa au kuomba kazi wakati barua za rejesta huandikwa kwa lengo la kuburudisha.

Katika Kielelezo Na. 7.3 mtahiniwa aliandika kuwa barua ya kawaida ni kwa lengo maalum na rejista kwa ajili ya kuburudisha badala ya kuandika tofauti za utumaji, upokeaji, aina ya bahasha na gharama za utumaji.

## 2.8 Swali la 8: Ufundishaji wa Mada za Mfano

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kupendekeza mbinu nne zinazoweza kutumika kufundishia mada ya usikivu kwa wanafunzi wa somo la TEHAMA.

Katika uchambuzi wa swali hili ilibainika kuwa, jumla ya watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa 4887 ambapo asilimia 60.3 walipata alama 0 hadi 1.5, asilimia 26.2 walipata alama 2 hadi 2.5 na asilimia 13.5 walipata alama 3 hadi 4, kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 8.1.




**Kielelezo Na. 8.1:** *Ufaulu wa Watahiniwa Swali la 8*

Uchambuzi huu umebaini kuwa Asilimia 60.3 ya watahiniwa walipata alama za chini (0 hadi 1.5). Hii inadhihirisha kuwa watahiniwa waliowengi hawakuwa na maarifa na umahiri wa kutosha katika kupendekeza mbinu zinazoweza kutumika kufundishia mada ya usikivu kwa wanafunzi wa somo la TEHAMA. Kwa mfano, mtahiniwa mmojawapo aliandika;

(i) Kutumia redio.
(ii) Kutumia vitabu.
(iii) Kutumia redio kaseti.
(iv) Kutumia magazeti.


Aidha, mtahiniwa mwingine aliandika kama ifuatavyo:

(i) Mbinu ya Onyesho mbinu.
(ii) Mbinu ya Kazi mradi.
(iii) Mbinu ya Ziara.
(iv) Mbinu ya kutumia vitabu.

Pamoja na majibu haya, uchunguzi uliofanyika kwa kupitia baadhi ya vijitabu vyao vya kujibia maswali umedhihirisha kwamba asilimia kubwa ya watahiniwa (60.3%) hawakuelewa swali hivyo, walichanganya hatua za ufundishaji na mbinu za ufundishaji. Baadhi ya watahiniwa waliandika; kuanza na utangulizi, kuuliza maswali juu ya mada ya usikivu, kuweka katika makundi ya majadiliano na kutoa mazoezi.

Aidha, mtahiniwa mwingine aliandika vifaa badala ya kutaja mbinu. Mtahiniwa huyo alitaja vifaa kama redio, kompyuta, runinga na magazeti. Kielelezo Na. 8.2 ni mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kupendekeza mbinu nne zinazoweza kutumika kufundishia mada ya usikivu kwa wanafunzi wa somo la TEHAMA.

**Kielelezo Na. 8.2**


8. Mbinu za kufundisha mada ya usikivu
a) Kutumia mbinu bora
b) Kutumia zana bora
c) Kuwashirikisha wanafunzi darasani
d) Kuwamotisha pale wanapofanya vizuri


Kielelezo Na. 8.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambaye alishindwa kupendekeza mbinu za ufundishaji, aliandika; kutumia mbinu bora, zana bora kuwashirikisha na kuwamotisha wanafunzi, badala ya; kwa njia ya maswali na majibu, nyimbo, hadithi na majadiliano.

Japokuwa watahiniwa wengi hawakujibu vizuri swali hili, wapo baadhi ya watahiniwa (39.7%) walioweza kujibu vizuri. Watahiniwa hawa waliweza kupendekeza kwa usahihi mbinu zinazoweza kutumika kufundisha kipengele cha usikivu katika somo la TEHAMA. Kwa mfano, mtahiniwa mmojawapo aliandika;

(i) Majadiliano katika vikundi.
(ii) Maswali na majibu.
(iii) Kualika mgeni.

Majibu haya yanaonesha kuwa watahiniwa hawa walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya mbinu zinazoweza kutumika kufundishia mada ya usikivu. Kielelezo Na. 8.2 ni mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo Na  8.3**


8. i) Majadiliano katika vikundi
hii mbinu itawafanya wanafunzi wasikilize
mawazo na kuyachambua ili waweze kuya-
wasilisha kwa ufasaha. kabla

ii) Mhadhara.
Ni mbinu ambayo itawafanya wanafunzi
wasikilize kwa makini ili wachambue
mawazo muhimu.

iii) Mbinu ya maswali na majibu;
kwani inawafikirisha wanafunzi na
kuwafanya watafakari kwa kina swali
lililoulizwa na kusikiliza kwa makini
majibu yao.


iv) Kualika mgeni.
Kama mgeni atafundisha mada ya usikivu
wanafunzi watasikiliza kwa makini
kwani watoto hupenda kupata maarifa
kutoka kwa mgeni huyo.

Katika Kielelezo 8.3 mtahiniwa aliweza kueleza njia ambazo zingefaa kutumika ili kuweza kufundisha mada hiyo ambazo ameziandika kuwa ni mhadhara, maswali na majibu na kualika mgeni.

## 2.9 Swali la 9: Upimaji

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kufafanua kwa ufupi aina kuu nne za upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi katika somo la TEHAMA.

Uchambuzi wa swali hili unaonesha kuwa watahiniwa 4887 walifanya swali hili. Asilimia 86.7 walipata alama 3 hadi 4, asilimia 7.3 walipata alama 2 hadi 2.5  na asilimia 6 walipata 0 hadi 1.5, kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 9.1.




**Kielelezo Na. 9.1:** *Ufaulu wa Watahiniwa Swali la 9*

Uchambuzi wa majibu ya swali hili unadhihirisha kuwa asilimia 94 ya watahiniwa wote walipata alama za juu ambazo ni alama 2 hadi 4. Majibu ya watahiniwa hawa yanaonesha kuwa waliweza kufafanua vizuri aina kuu za upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi kulingana na matakwa ya swali. Baadhi ya majibu sahihi ya baadhi ya watahiniwa yaliyopatikana kwenye vijitabu vyao vya kujibia ni kama yafuatayo:

(i) Upimaji wa awali: Upimaji huu hufanyika mwanzoni.
(ii) Upimaji endelevu: Upimaji huu hufanyika katika kipindi chote cha mafunzo.
(iii) Upimaji tatuzi: Upimaji huu hufanyika kwa lengo la kutatua matatizo waliyonayo wanafunzi.
(iv) Upimaji tamati: Upimaji huu hufanyika mwishoni mwa mafunzo.

Majibu haya yanadhihirisha kuwa watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina za upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi. Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kufafanua kwa ufupi aina kuu nne za upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi katika somo la TEHAMA.

**Kielelezo Na. 9.2**


9. i) Upimaji wa awali. Huu hufanywa kama
tu mwanafunzi aingiapo shuleni ili
kujua kama atawera kumudu stadi zo
aina mbalimbali atakazo fundishwa.
ii) Upimaji endelevu. huu hufanyika muda
wote mwanafunzi anapojifunza somo la
TEHAMA ili kujua maendeleo yake katika
kujifunza kwake. mfano mazoezi na ma-
jaribio huu ni upimaji endelevu
iii) upimaji tatuzi. Huu hufanywa ili kubaini
matatizo alizonayo mwanafunzi katika
ujifunzaji wa somo la TEHAMA ili kuyata-
futia ufumbuzi
iv) upimaji tamati. huu hufanywa mwishoni
ili kujua kama mwanafunzi amewera kufi-
kia lengo lililokusudiwa katika ujifunzaji wa
somo la TEHAMA mfano kutoa mtihani


Katika Kielelezo Na. 9.2 mtahiniwa aliweza kubainisha aina za upimaji ambazo ni awali, endelevu, tatuzi na tamati pamoja na muda wa kutumika.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (6.0%) hawakujibu vizuri swali hili. Watahiniwa hawa walipata alama 0 hadi 1.5. Majibu yao yanaonesha kuwa hawakuwa na maarifa ya aina za upimaji. Baadhi ya watahiniwa walitaja njia zinazotumika kumpima mwanafunzi, kama vile:

(i) Maswali.
(ii) Mazoezi.
(iii) Majaribio.
(iv) Mitihani.

Aidha, wengine walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Majibu haya yanaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu *Upimaji*. Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alishindwa kutofautisha kati ya zana za upimaji na aina za upimaji.

**Kielelezo Na. 9.3**




Katika Kielelezo Na. 9.3 mtahiniwa alishindwa kubainisha aina za upimaji na muda wa kutumika ambazo ni awali, endelevu, tatuzi na tamati. Yeye aliandika; mazoezi, mitihani, majaribio na jedwali la utahini badala ya kufafanua aina za upimaji.

## 2.10 Swali la 10: Maandalizi ya Ufundishaji

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kubainisha njia nne zinazoweza kumsaidia mwalimu wa somo la TEHAMA kupata zana za kufundishia na kujifunzia.

Uchambuzi wa swali hili unaonesha kuwa, jumla ya watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa 4887 ambapo, asilimia 6 walipata alama 0 hadi 1.5,

asilimia 50.7 walipata alama 2 hadi 2.5 na asilimia 43.3 walipata alama 3 hadi 4. Swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa asilimia 94 kwani watahiniwa walipata alama 2 hadi 4, kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.10.1.




**Kielelezo Na. 10.1***: Ufaulu wa Watahiniwa Swali la 10*

Katika swali hili asilimia 94 ya watahiniwa waliweza kubainisha njia mbili mpaka nne zinazoweza kumsaidia mwalimu wa somo la TEHAMA kupata zana za kufundishia na kujifunzia. Majibu haya ya watahiniwa katika swali hili yanadhihirisha kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu utengenezaji wa zana za kufundishia.Yafuatayo ni baadhi ya majibu kutoka kwa mmoja wa watahiniwa:

(i) Kwa njia ya kununua: Mwalimu anaweza kupata zana kwa njia ya kununua dukani, mfano, redio na kompyuta.

(ii) Kwa njia ya kuokota: Mwalimu anaweza kuokota zana mbalimbali katika mazingira yake.

(iii) Kwa njia ya kuazima: Mwalimu anaweza kuazima kompyuta kutoka shule jirani.

(iv) Kwa njia ya kufaragua na kutengeneza: Mwalimu anaweza kutengeneza kifani cha simu au redio kwa kutumia maboksi.

Uchambuzi wa majibu haya unaonesha kuwa watahiniwa hawa walikuwa na maarifa na umahiri wa kutosha kuhusu *Ufundishaji wa Mada za Mfano*. Kielelezo Na. 10.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo Na. 10.2**

10. Mwalimu wa TEHAMA anaweza kupata zana za kufundishia na kujifunzia katika njia zifuatazo:
(i) Njia ya kununua, mwalimu anaweza kununua vifaa vya kufundishia dukani kama kununua redio kwa ajili ya kufundishia mada ya Usikivu.
(ii) Njia ya kuazima, pia mwalimu anaweza kuazima zana, kama kuazima kompyuta kufundishia programu jedwali na programu andishi.
(iii) Njia ya kubuni/kutengeneza na kutengeneza, pia mwalimu anaweza kutumia malighafi zilizo halisi au zisizo halisi kutengeneza zana za kufundishia.
(iv) Njia ya kuokota, pia Mwalimu anaweza kutumia njia ya kuokota vikombe au zana yoyote kama mkopo na kutumika kama zana kufundishia ya mambo ya vitu mbalimbali katika somo la TEHAMA.

Katika Kielelezo Na. 10.2 mtahiniwa alibainisha njia zinazoweza kumsaidia mwalimu kupata zana za kufundishia na kujifunzia ambazo ni; kununua, kuazima, kubuni na kuokota.

Kwa upande mwingine, baadhi ya watahiniwa (6%) waliopata alama 0 hadi 1.5, majibu yao yanaonesha kuwa hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya njia zinazoweza kumsaidia mwalimu wa somo la TEHAMA kupata zana za kufundishia na kujifunzia. Pia, watahiniwa walishindwa kuelewa matakwa ya swali, ambapo walitaja tu bila kubainisha au kutoa maelezo kwa ufupi na wengine kuandika majibu ambayo yako ndani ya kipingele kimoja cha jibu kama vile kuchonga, kusuka na kufinyanga. Baadhi ya majibu yao yalikuwa kama ifuatavyo:

(i) Mada husika.
(ii) Walengwa au umri wa walengwa.
(iii) Malengo ya somo.
(iv) Mbinu au njia za kufundishia na kujifunzia.

Mtahiniwa mwingine alijibu kama ifuatavyo*:*

(i) Kuchora.
(ii) Kufinyanga.
(iii) Kusuka.

Uchambuzi wa majibu haya unaonesha kuwa watahiniwa hawa walikosa maarifa ya *Maandalizi ya Ufundishaji* hasa zana za kufundishia. Kielelezo Na. 10.3 ni mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili.

**Kielelezo Na. 10.3**



10. i, Kufinyanga.
ii, Kusuka.
iii, Kuchora.
iv, Kukusanya.

Katika Kielelezo Na. 10.3 mtahiniwa aliandika; kufinyanga, kusuka, kuchora; badala ya kununua, kuazima, kubuni na kuokota.

## 2.11 Swali la 11: Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji Somo la TEHAMA

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kujadili mambo matano yanayoweza kuonesha ubaguzi wa kijinsia wakati wa ufundishaji na ujifunzaji somo la TEHAMA.

Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 3379 sawa na asilimia 100, ndio waliojibu swali hili. Aidha, asilimia 56.4 walipata alama 10.5 hadi 15, asilimia 41.2 walipata alama 6 hadi 10 na asilimia 2.4 walipata alama 0 hadi 5.5. Kwa ujumla, kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwani asilimia 97 ya watahiniwa walipata alama zaidi ya 5.5, kama ilivyooneshwa kwenye Kielelezo Na. 11.1.




**Kielelezo 11.1:** *Ufaulu wa Watahiniwa Swali la 11*

Uchambuzi uonaonesha kwamba asilimia 97.6 ya watahiniwa waliweza kujadili kwa usahihi mambo yanayoweza kuonesha ubaguzi wa kijinsia wakati wa ufundishaji na ujifunzaji somo la TEHAMA. Hii inadhihirisha kuwa watahiniwa hawa walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya ubaguzi wa kijinsia. Baadhi ya majibu ya watahiniwa waliojibu vizuri swali hili ni kama ifuatavyo:

(i) Kutumia picha na michoro inayoonesha jinsia moja kubaguliwa.
(ii) Kutenganisha jinsia kwenye kazi zinazofanywa na vikundi.
(iii) Kutumia lugha ya kibaguzi inayobagua upande mmoja.
(iv) Kutokutoa nafasi sawa katika uongozi kwa kupendelea jinsia moja tu kuwa viongozi darasani.
(v) Kupendelea kuchagua jinsia moja wakati wa kujibu maswali.


Aidha, mtahiniwa mwingine aliandika hivi*;*

(i) Kutozingatia usawa katika kugawa vifaa vya kufundishia na kujifunzia TEHAMA.
(ii) Kutozingatia mkao wa darasa katika jinsia.
(iii) Kutozingatia usawa katika kutoa nafasi ya kuuliza au kujibu maswali.
(iv) Kutozingatia usawa katika kupanga vikundi.

Usahihi wa majibu yaliyotolewa na watahiniwa unadhihirisha kuwa watahiniwa hawa walikuwa na uelewa mzuri wa mambo yanayoweza

kuonesha ubaguzi wa kijinsia. Kielelezo Na. 11.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu vizuri swali hili.

**Kielelezo Na. 11.2**



11 Ubaguzi wa kijinsia ni kitendo cha kupendelea jinsia moja kwa kuona inaweza sana kuliko jinsia nyingine. Yafuatayo ni mambo yanayoweza kuonesha ubaguzi wa kijinsia wakati wa ufundishaji na ujifunzaji.

Kutumia picha au michoro inayoonesha jinsia moja inabaguliwa mwalimu anapotumia picha au michoro mbalimbali inayoonesha jinsia moja inabaguliwa ni kama kwa watoto inakuwa nafasi ulali wa jinsia kutopendelea kwa jinsia inayobaguliwa kuona kama haitendewi haki mfano mwalimu anapotumia picha ya mama amebeba mizigo mingi pamoja na mtoto huku baba anatembea bila kuwa na mzigo wowote.

Kutenganisha jinsia kwenye kazi za vikundi wanazofanya pia mwalimu anapokuwa anatoa kazi za vikundi akatenganisha jinsia kila moja akatakiwa peke yake inakuwa ni ubaguzi wa jinsia kwasababu itapelekea kwa wanafunzi wale kujiona kila mjinsia ni bora kuliko nyingine pakofanya kuiwe na ubaguzi wa wakati wa ufundishaji na ujifunzaji.

Kutumia lugha ya kibaguzi inayobagua upande mmoja pia mwalimu anapokuwa anafundisha darasa akatumia lugha ya kibaguzi kwa kubagua jinsia moja ni chanzo cha kuonesha ubaguzi wa jinsia wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Mfano mwalimu anatumia lugha ya kebehi kwa wasichana au wavulana kati yao wajinga.

Kutotoa nafasi sawa katika uongozi kwa kupendelea jinsia moja tu kuwa viongozi darasani pia mwalimu anapashindwa kutoa nafasi sawa katika kuchagua viongozi na kupendelea jinsia moja tu kwa kuona inaweza sana kuliko jinsia nyingine nikosa kubwa na nichanzo cha

Katika Kielelezo Na. 11.2 Mtahiniwa aliweza kueleza kwa usahihi mambo yanayoweza kuonesha ubaguzi wa kijinsia wakati wa ufundishaji na ujifunzaji somo la TEHAMA. Aliandika; matumizi ya picha zenye kuashiria ubaguzi, ugawaji wa makundi ya kujifunzia, matumizi ya lugha ya kibaguzi, na utoaji wa nafasi katika shughuli mbalimbali.

Pamoja na watahiniwa wengi kufanya vizuri swali hili, wapo watahiniwa wachache waliojibu vibaya. Majibu ya watahiniwa hawa yalionesha kuwa watahiniwa hawa hawakuwa na maarifa yakutosha kuhusu mambo yanayoweza kuonesha ubaguzi wa kijinsia. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika;

(i) Nidhamu: Katika suala zima la ufundishaji na ujifunzaji nidhamu ni kitu cha muhimu sana kwa sababu mwanafunzi asipokuwa na nidhamu katika kujifunza inaweza ikawepo ubaguzi wa kijinsia.
(ii) Mahusiano ya kijinsia: pia hii inaweza kutokea endapo mwalimu na mwanafunzi wana mahusiano ya kijinsia inaweza kupelekea kuwepo kwa ubaguzi wa kijinsia.
(iii) Makundi mabaya: Endapo katika suala zima la ufundishaji na ujifunzaji, kuna wanafunzi kati yao wana tabia mbaya ambazo haziendani na wanafunzi wengine kuna uwezekano mkubwa wa kuwepo kwa ubaguzi wa kijinsia.
(iv) Tabia mbaya ya wanafunzi, pia hii inaweza kupelekea kuwepo kwa ubaguzi wa kijinsia katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji.


Mtahiniwa mwingine alishindwa kubaini maana halisi ya ubaguzi wa kijinsia, hivyo aliandika kuhusu kunyanyapaa na hali za wanafunzi. Yafuatayo ni majibu ya mtahiniwa huyo*:*

(i) Ulemavu wa viungo mbalimbali.
(ii) Wanafunzi wenye matatizo ya kiakili.
(iii) Mwanafunzi kuwa na uwezo mdogo.
(iv) Mwanafunzi kuwa mchafu.
(v) Mwanafunzi kuwa mtoro.

Uchambuzi uliofanyika unaonesha kuwa watahiniwa walikosa maarifa juu ya *Misingi ya Ufundishaji Somo la TEHAMA*. Kielelezo Na. 11.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakuweza kujibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo Na. 11.3**

11 Ubaguzi wa Kijinsia katika somo la te
hama ni hali ya kundi moja kupata hu
duma stahiki pasipo kwa kulingani sha na
kundi jingine mfano wenye mahitaji ma
lumu yaani, noni hafifu wasiosikia. Hivyo
ubaguzi huu hutokana na mambo yafuatayo
Ufundishaji usio zingatia hali wa jinsia
katika ufundishaji wa somo la tehama -
Mwalimu asipo zingatia ~~uhali~~ hali wa jinsia
mfano kwa wenye mahitaji maalumu yani wa
sio sikia wenye uelewe mkubwa na mdogo.
Ufundishaji usio zingatia matumizi
yazana, katika ufundishaji baadhi ya wa
nafunzi huelewa kwa kutumia zana ambazo
huwapa udadisi na uelewa wa kujua ya somo
Ufundishaji usio zingatia idadi ya
wanafunzi hii hwonye kuwa katika ufu
ndishaji lazima Mwalimu aweze kutu
mia ~~zana~~ idadi ya wanafunzi ili kutunge
neza zana bora ni ~~za~~ zinazo jitosheleza ka
tika darasa husika.
Ufundishaji usio zingatia umri wa
wanafunzi ili kuondoa hali ya ubaguzi
Mwalimu lazima aweze kuzingatia umri
wa wanafunzi anao wafundisha ili aweze
kutumia mbinu nayo wafaa katika ufu
ndishaji wa somo.
Ufundishaji usiozingatia uelewa
wa wanafunzi mfano mwalimu kuwa mse
maji bila kumpa mwanafunzi nafasi ya




Kuchagua mwanzo yake ili akithimini ni
Kiasi gani wanafunzi wameelewa
Hivyo Mambo yanayoweza kututua
aukaondoa ubaguzi ukiwa kama mwalimu
lazima awe Kutambua na Kuelewa vizu
ri darasa analo lifundisha ilo Katambua na
umbile na uelewa wanafunzi darasani

Kielelezo Na. 11.3 ni sampuli ya mtahiniwa aliyeandika kuhusu vigezo vya mwalimu katika ufundishaji kuwa ni umri, uwezo wa wanafunzi, matumizi ya zana na idadi ya wanafunzi badala ya upendeleo, michoro, lugha na matumizi ya video.

## 2.12 Swali la 12: Ufundishaji wa Mada za Mfano

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa kina mambo matano yanayoweza kuathiri uwasilishaji wa habari iliyosemwa.

Uchambuzi uliofanyika ulibainika kuwa watahiniwa 1817 sawa na asilimia 100 walifanya swali hili. Asilimia 9.4 walipata alama 0 hadi 5.5, asilimia 73.4 walipata alama 6 hadi 10 na asilimia 17.2 walipata alama 10.5 hadi 15. Uchambuzi huu unaonesha kuwa kiwango cha ufaulu kilikuwa kizuri kwani asilimia 90.6 walipata alama 6 hadi 15 kama ilivyooneshwa katika Kielelezo Na.12.1.




**Kielelezo Na. 12.1**: *Ufaulu wa Watahiniwa Swali la 12*

Uchambuzi uliofanyika katika swali hili unaonesha kuwa asilimia 90.6 ya watahiniwa walikuwa na maarifa na umahiri wakutosha kuhusu mambo

yanayoweza kuathiri uwasilishaji wa habari iliyosemwa. Majibu sahihi ya baadhi ya watahiniwa yaliyopatikana kwenye vijitabu vyao vya kujibia yameainishwa kama ifuatavyo:


(i) Kutokuwepo umakini wakati wa kupokea habari.
(ii) Lugha iliyotumika: Endapo lugha iliyotumika wakati wa kutoa taarifa ni ngumu na haieleweki kwa wasikilizaji.
(iii) Dosari katika viungo vya mwili: Kama msikilizaji atakuwa na dosari katika viungo vyake vya mwili vitakavyomhusisha kusikia na kuzungumza.
(iv) Taarifa iliyosemwa huweza kuathiriwa endapo kutakuwepo na kelele.
(v) Taarifa hutegemea njia iliyotumika ili kuifanya taarifa kuwa na ufasaha kama msemaji atashindwa kutumia njia sahihi za mawasiliano.

Vile vile, mtahiniwa mwingine katika kulijibu swali hili aliandika mambo yafuatayo:

(i) Kupunguza au kuongeza maneno.
(ii) Kutokuwepo na usikivu.
(iii) Kutoandaa dondoo.
(iv) Kutokuwa makini wakati wa kusikiliza.

Majibu ya watahiniwa hawa yanaonesha kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha katika *Ufundishaji wa Mada za Mfano* hasa uwasilishaji wa habari iliyosemwa. Kielelezo Na. 12.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kueleza vizuri mambo matano yanayoweza kuathiri uwasilishaji wa habari iliyosemwa.

**Kielelezo Na. 12.2**


12. Uwasilishaji wa habari ni kitendo cha kusema
taarifa ambayo tayari ilishazungumzwa. Hivyo
mambo yafuatayo yanaweza kuathiri uwasilishaji
wa habari iliyosemwa.
Kusahau, mtu anapolipokea jambo au taarifa
au habari yoyote bila kuandika sehemu yoyote
upo uwezekano mkubwa wa kusahau baadhi ya
mambo wakati wa kueleza habari au taarifa
iliyosemwa

Athari za lugha mama, kuathiriwa kwa,
lugha mama huweza pia kusababisha mtu ku
shindwa kuwasilisha habari iliyoelewa-
kwa usahihi kutokana na kushindwa kutamka
baadhi ya maneno kwa usahihi.

Kutozingatia matamshi sahihi ya maneno, hu
sababisha mtu kushindwa kuwasilisha habari ili
yosemwa. namna ya kutamka baadhi ya mane
no baadhi ya watu hushindwa na unaweza ku
sema neno likawa na maana tofauti na kilicho
maanishwa

Matatizo ya kisembe, kwa baadhi ya watu
wamekosa ala za sauti na hivyo kushindwa kuta
mka maneno kwa ufasaha. Kwa mfano alinun
ua vitu vya thamani kubwa. mtu anaweza-
kusema samani badala ya thamani tayari ame
badilisha maana

Kigugumizi hili ni tatizo la mtu kushindwa
kupangilia maneno au kuvuta maneno wakati-
wa kuzungumza. Hivyo hii ni changamoto kati
ka uwasilishaji wa habari iliyosemwa na kusaba
bisha muwasilishaji asieleweke.

Katika Kielelezo Na. 12.2 mtahiniwa aliandika mambo yanayoathiri uwasilishaji wa habari iliyosemwa kwa usahihi; ambayo ni adhari za kimaumbile hasa wenye matatizo ya kigugumizi na kidhembe, uwezo wa kusikia na mazingira ya upokeaji wa habari hiyo**.**

Hata hivyo, asilimia 9.4 ya watahiniwa walishindwa kujibu swali hili vizuri kutokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu uwasilishaji wa habari iliyosemwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika;


(i) Habari haiwezi kufikiwa kwa usahihi kwa sababu mtu aliyesema habari hiyo atakuwa siyo mhusika, anaweza kupunguza au kuongeza maneno.
(ii) Habari kutoeleweka vizuri, hivyo anayepelekewa taarifa hushindwa kujua afanye nini ili aweze kupata taarifa zaidi.
(iii) Pia ugomvi unaweza kutokea baina ya pande mbili hasa mtoa habari na yule aliyesimulia hiyo habari.


(iv) Mtoa habari anaweza kusahau ile habari aliyoambiwa akaitoe hivyo kusababisha habari hiyo kutomfikia mlengwa.

(v) Pia mtoa habari akifa pengine kutokana na ajali mbalimbali, mfano ajali ya gari, hivyo taarifa iliyokusudiwa haiwezi kumfikia.

Majibu haya yanadhihirisha kuwa watahiniwa hawa walikosa maarifa ya *Ufundishaji wa Mada za Mfano* hasa uwasilishaji wa habari iliyosemwa. Kielelezo Na. 12.3 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi kutoka kwa mtahiniwa mmojawapo.

**Kielelezo Na. 12.3**


12. Uwasilishaji wa habari. Ni kitendo kiboa taarifa iliyokusudiwa zeimwa kwa mara ya pili. Yafuatayo ni mambo yanayoweza kuharibu uwasilishaji wa taarifa iliyosemwa.
Kupotea kwa chombo / kifaa kilichohifadhiwa mfano taarifa hiyo ilikuwa imehifadhiwa kwenye simu na simu hiyo kupotea huweza kuharibu uwasilishaji wa taarifa.
Kifaa kuharibika. Mfano taarifa iliyohifadhiwa au kuhifadhiwa kwenye tarakilishi huweza kupotea endapo tarakilishi hicho kitaka zoharibika.
Moto. Moto huweza kuharibu taarifa kwa kifaa hicho kuungua kwa sehemu ndogo au chote kuungua.
Maji. mfano taarifa iliyohifadhiwa kwenye simu huweza kuharibika endapo simu hiyo itazama kwenye maji
Vumbi. Vumbi huweza kuharibu uwasilishaji wa taarifa iliyosemwa kwa



mfano C.D. Itakapopata vumbi huweza
kuharibika na huyo taarifa iliyopo
kushindikana kuwasilishwa ipasavyo. lakini
taarifa zote huweza kuharibika kutoka
kana na kifaa kilichotumika kuhifadhia
kupata kutokana hitilafu mbalimbali mfano
umeme.

Katika Kielelezo Na. 12.3 mtahiniwa aliandika kuhusu kutokuwepo kwa chombo, kifaa kuharibika, moto, maji na vumbi; badala ya lugha, maumbile na maneno kuwa na maana zaidi ya moja.

## 2.13 Swali la 13: Ufundishaji wa Mada za Mfano

Katika swali hili watahiniwa walitakiwa kutathmini mchango wa mtandao wa intaneti katika kuleta msawazo wa mawasiliano katika jamii.

Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 2459 sawa na asilimia 100 walifanya swali hili ambapo asilimia 2.3 walipata alama 0.5 hadi 5.5, asilimia 73.2 walipata alama 6 hadi 10 na asilimia 24.5 walipata alama 10.5 hadi 15 Uchambuzi huu umeonesha kuwa swali hili lilifanyika vizuri kwani asilimia 97.7 ya watahiniwa walipata zaidi ya alama 5.5. Kielelezo Na. 13.1 kinaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili kwa ufupi.




**Kielelezo Na. 13.1**: *Ufaulu wa Watahiniwa Swali la 13*

Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa waliojibu swali hili kwa usahihi waliweza kutathmini mchango wa mtandao wa intaneti katika kuleta msawazo wa mawasiliano katika jamii. Majibu ya watahiniwa yanaonesha

kuwa watahiniwa wengi (97.7%) walielewa vizuri mchango wa mtandao wa intaneti ambayo inadhihirisha kwamba watahiniwa hawa walikuwa na maarifa yakutosha juu ya swali hili. Baadhi ya majibu sahihi ya mmoja wa watahiniwa ni kama ifuatavyo:

(i) Husaidia kuelimisha jamii: Mtandao wa intaneti umesaidia sana kuwaelimisha watu kutokana na kupata taarifa au habari kutoka maeneo mbalimbali ya kiulimwengu.
(ii) Husaidia katika kupashana habari: Hii ni kwamba, mtandao wa intaneti umechangia sana watu kupashana habari kutoka sehemu moja kwenye nyingine kwa kutumia mitandao mfano facebook, whatsapp na instagram.
(iii) Hujenga ushirikiano na mahusiano mema miongoni mwa wanajamii.
(iv) Hutusaidia kutupatia ajira: Hii ni kwamba mtu anapokuwa na utaalam katika mtandao husika humsaidia kutoa huduma ya kuwasaidia watu kupitia mtandao huo.
(v) Hutusaidia kupata kipato na pia kuinua uchumi wa nchi.


Majibu ya baadhi ya watahiniwa hawa yanaonesha kuwa wanaelewa mchango wa mtandao wa intaneti katika kuleta msawazo wa mawasiliano. Kielelezo Na. 13.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyeweza kutathmini kwa usahihi mchango wa mtandao wa intaneti katika kuleta msawazo wa mawasiliano katika jamii.

**Kielelezo Na. 13.2**

13' Kutathmini Mchango wa Mtandao wa intaneti Katika Kuleta Msawazo wa Mawasiliano katika Jamii

MAJIBU

Mtandao wa intaneti ni Mtandao ambao hutoa habari mbalimbali kwa kutumia njia mbalimbali: Zifuatazo ni faida au Mchango wa Mtandao wa Intaneti katika Uwasilishaji au Msawazo wa Mawasiliano katika Jamii


Husaidia katika Upatikanaji wa habari mbalimbali: Mtandao wa intaneti husaidia katika upatikanaji wa habari mbalimbali katika jamii mfano kupitia simu, Luninga ambayo husaidia katika upatikanaji wa habari mbalimbali za kielimu kupitia simu, Luninga n.k.

Husaidia katika kurahisisha Mawasiliano: Mtandao wa intaneti ni muhimu, kwa sababu umesaidia katika upatikanaji wa kurahisisha mawasiliano mbalimbali katika jamii kupitia simu.

Husaidia katika kuongeza ufanisi wa kazi: Mtandao wa intaneti ni muhimu kwa sababu husaidia katika kuongeza ufanisi wa kazi na kuleta msawazo wa Mawasiliano kutokana na kompyuta ambayo husaidia katika uchapaji wa makala mbalimbali za kiofisi.

Husaidia katika kuokoa muda kwa kusambaza nyaraka za kazi kwa wakati; huu ni mchango wa Mtandao wa intaneti ambao umesaidia katika kusambaza nyaraka za kazi kwa wakati na kuleta msawazo wa Mawasiliano katika ki jamii kupitia kompyuta au simu ambayo husaidia kuokoa muda.

Kielelezo Na. 13.2 kinaonesha kuwa mtahiniwa alieleza mchango wa mtandao wa intaneti kama; husaidia upatikanaji wa habari, mawasiliano, ufanisi na kuokoa muda.

Kwa upande mwingine, asilimia 2.3 ya watahiniwa walishindwa kutoa tathmini ya mchango wa mtandao wa intaneti katika kuleta msawazo wa mawasiliano katika jamii kutokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada hii. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika;

Kuepusha gharama katika mawasiliano, kupata ufumbuzi wa tatizo na kuleta madhara kwa jamii kwa mfano kuvunjika kwa maadili. Vile vile mtahiniwa mwingine aliandika; kupunguza gharama na kutunza siri. Kielelezo Na. 13.3 ni mfano wa jibu la mtahiniwa ambaye hakuweza kutathmini mchango wa mtandao wa intaneti katika kuleta msawazo wa mawasiliano katika jamii.

**Kielelezo Na. 13.3**

13. Mtandao wa inteneti ni mkusanyiko wa vifaa mbalimbali ambayo vinatoa uwezo wa kompyuta kuwasiliana.

Mtandao wa inteneti huleta changamoto katika mawasiliano katika jamii, changamoto hizo ni kama ifuatavyo;

Kutoa taarifa zenye kuleta uchochezi, matumizi ya mtandao wa inteneti huleta machafuko katika jamii kwa kusambaza taarifa zinazochochea uvunjifu wa amani katika jamii, hii ni kutokana na watu kutumia mitandao vibaya bila kufikiri madhara ambayo yanaweza kutokea mfano, hapa Tanzania mwalimu mmoja wa chuo kikuu Dar-es-Salaam alisambaza ujumbe wa kuandamana nchi nzima ambayo yalisababisha kuleta hofu kwa wananchi.

Wizi wa mtandaoni, matumizi mabaya ya mtandao watu baadhi hutumia ili kujinufaisha kwa kutumia mitandao kulaghai watu mfano wizi wa fedha katika mitandao mbalimbali.

Ugaidi, wahalifu hutumia mtandao kufanya maovu ambayo huleta madhara kwa watu kwa kuweka mtandao wa uhalifu katika sehemu mbalimbali. Mfano kuweka programu ambazo zinatumwa kwa njia ya mtandao na kuleta madhara baada ya kufungua ujumbe ambao umetumwa katika mtandao.


Katika Kielelezo Na. 13.3 mtahiniwa aliandika; hutoa taarifa za uchochezi, wizi wa mtandaoni na ugaidi; badala ya kuandika; kupata taarifa na habari, kuburudisha, biashara, elimu na matangazo.

## 2.14 Swali la 14: Upimaji

Katika swali hili, watahiniwa walitakiwa kutoa mifano na kufafanua nyanja zozote tano za utambuzi kwa mujibu wa mtaalamu Benjamin Bloom zinavyotumika katika upimaji wa maendeleo ya wanafunzi.

Uchambuzi unaonesha kwamba watahiniwa 2983 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Asilimia 3.5 walipata alama 0 hadi 5.5, asilimia 58.4

walipata alama 6 hadi 10 na asilimia 38.1 walipata alama 10.5 hadi 15. Kwa ujumla swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwani asilimia 96.6 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama 6.0 hadi 15.0 kama, ilivyooneshwa kwenye Kielelezo Na. 14.1.




**Kielelezo Na. 14.1**: *Ufaulu wa Watahiniwa Swali la 14*

Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa waliopata alama 6 hadi 15 walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya nyanja za upimaji kwani waliweza kutoa mifano na kufafanua nyanja za utambuzi kwa mujibu wa mtaalamu Benjamin Bloom zinavyotumika katika upimaji wa maendeleo ya wanafunzi. Kwa mfano, baadhi ya majibu ya mmojawapo wa watahiniwa waliofanya vizuri swali hili kwenye vijitabu vyao vya kujibia aliandika kama ifuatavyo:

(i) Maarifa: Nyanja hii ya utambuzi huangalia zaidi kumbukumbu alizonazo mwanafunzi katika kujifunza, mfano kutumia maarifa aliyonayo katika kutatua matatizo yanayomkabili katika kujifunza kwake.

(ii) Ufahamu: Hii hutumika kupima mwanafunzi uwezo wa kufikiri kwa kina mambo anayojifunza mfano kufupisha habari au kueleza jambo kwa ufupi.

(iii) Matumizi: Hii ni nyanja mojawapo ya utambuzi ambayo humpima mwanafunzi jinsi ya kutumia stadi mbalimbali katika kutafuta jibu. Kwa mfano, kwa kutumia kanuni kutafuta eneo la pembe tatu.


(iv) Uchambuzi: Hii ni nyanja ambao mwanafunzi hupimwa uwezo wa kutofautisha mambo anayojifunza kutokana na kubadilika kwake kama vile, tofautisha kati ya seli ya mmea na seli ya mnyama.

(v) Uundaji: Ni kitendo cha kubuni na kuunganisha mawazo na kuweka pamoja kwa mfano, mwanafunzi katika ngazi hii ya uundaji hupimwa jinsi anavyoweza kuhusianisha wazo alilojifunza ili kupata wazo jingine.

Kwa upande mwingine, katika swali hili watahiniwa waliowengi (96.5%) walipata alama za juu (6 hadi 15) kwasabau waliweza kutaja na kutoa mifano katika nyanja za utambuzi kulingana na matakwa ya swali. Baadhi yao walitoa mifano katika baadhi ya nyanja hali iliyosababisha watahiniwa hao kupata alama za wastani (6 hadi 10). Kielelezo Na. 14.2 ni sampuli ya jibu sahihi kutoka kwa mmoja kati ya watahiniwa waliweza kutoa mifano na kufafanua nyanja za utambuzi kwa mujibu wa Benjamin Bloom.

**Kielelezo Na. 14.2**

14. Utambuzi ni nyanja inahusu Masuala ya Kitaaluma. Nyanja hii huhusika moja kwa moja na Masuala ya Elimu.
Zifuatazo ni nyanja tano zinazounda utambuzi
Maarifa, hii ni nyanja ya utambuzi ambayo hupima uwezo wa mwanafunzi kukumbuka mambo aliyojifunza. mfano Mwanafunzi kuweza kueleza dhana aliyojifunza kwa kipindi fulani
Ufahamu, Nyanja hii hupima namna ambavyo mwanafunzi analielewa jambo fulani ambalo huenda hajajifunza. mfano kumtaka mwanafunzi kueleza jambo fulani ambalo unataka kufundisha kwa siku hiyo.



Matumizi, Hii ni nyanja ambayo huchunguza-
uwezo wa mwanafunzi kutumia kanuni au-
dhana mbalimbali alizojifunza katika masuala
ya Elimu. mfano kupima uwezo wa mwanafunzi
kutumia kanuni katika kufanya maswali fulani
Uchambuzi, Hii ni nyanja ambayo huangali
a uwezo wa mwanafunzi kuchambua masuala
mbalimbali ya kitaaluma mfano kuwez.. -
kuchambua masuala ya kielimu na masuala me
ngine mfano siasa au utandawazi
Uundaji, Hii ni nyanja ya utambuzi ambayo
huhusika na mwanafunzi kuunda kanuni au -
njia mbalimbali ambazo zitamuwezesha katika masuala
ya kufanikisha taaluma.
Hivyo basi, nyanja ya utambuzi inaumuhimu na -
mchango mkubwa sana katika suala la Elimu,

Katika Kielelezo Na.14.2 mtahiniwa aliweza kutoa mifano na kufafanua nyanja tano za utambuzi usahihi kwa kulingana na matakwa ya swali.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wengine (3.5%) hawakuweza kutoa mifano na kufafanua nyanja tano za utambuzi kutokana na kutoelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika;

(i) Ubunifu: Nyanja ya ubunifu hii katika upimaji hupimwa baada ya mwanafunzi kujitambua katika kujifunza kuwa ana ubunifu gani.
(ii) Uwezo wa kiakili na ufikirishwaji: Hii ni katika kufikiria baada ya mwanafunzi kujitambua na kufikiria hatua ya kupimwa, upimaji ufanyike kwa lengo kujua uwezo wake wa kiakili.
(iii) Utendaji: Pia katika mwanafunzi kujitambua na kufikia hatua ya kupimwa lengo ni kufahamu uwezo wake katika kutenda.

Majibu haya yanaonesha kuwa watahiniwa hawa walikosa maarifa ya *Upimaji* Kielelezo Na. 14.2 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo Na. 14.3**


hp Upimaji; Ni kitendo cha kutafuta ni kazi gani mwana
funzi ameweza kupata maarifa na stadi zinazowezdana /kuf
uatana na mada zilizopo katika muhtasari wa somo.
Utambuzi unaweza kutumika katika upimaji wa mwan
afunzi kwa kuangalia.
Upokeaji wa jambo; Hili ni moja katika kupima
utambuzi au katika nyanja za utam/ utambuzi nyanja
hii ya upokeaji wa jambo imesaidia katika kupima
fikra za mwanafunzi pale anapopewa kazi au maelezo hu
wa anahipokeaje jambo hilo kama mwanafunzi amelipokea
kwa uzuri basi atalifanyia kazi na kama mwanafunzi
hajalipokea kwa uzuri haitakuwa rahisi kulifanyia
kazi kwa maana hiyo baada ya kuwapa kazi aidha
ya darasani au njee ya darasa utapata majibu baada
ya kuona mwanafunzi alivyolipokea jambo hilo.
Uthamini wa jambo; Hili pia husaidia katika kupi
ma ambayo ipo katika nyanja ya utambuzi na hili
litatokea baada ya kumpa mwanafunzi maelekezo au
kazi yoyote au umempa ushauri wa kufanya jambo
au kumpa matatizo yako kwa kumpima tu baada
ya kufanya hivo utatambua je mwanafunzi huyo
anathamini utu au ukimwambia huwa akipokea kili
huwa anaonyesha uthamani wa utu au mambo hayo
hivyo ndipo utatambua mwanafunzi anaethamini jam
bo au anayelipuuzia jambo.
Mwelekeo; Katika kumpima mwanafunzi katika nyan
ja ya utambuzi pia mwelekeo husaidia kumpima m
wanafunzi hii hutokea pale mwalimu anapompa mwa
nafunzi maelezo au taarifa fulani apeleke mahali au
akafundishe wenzake na kuwaelekeza je tofauti na
kuwa na ~~mwelekeo~~ uthamini na hilo jambo je ana
mwelekeo wa kwenda kuelimisha wenzake ili hao

Katika Kielelezo Na. 14.3 mtahiniwa aliandika; upokeaji wa jambo, uthamini wa jambo na mwelekeo; badala ya kuandika; maarifa, ufahamu, matumizi, uchambuzi, uundaji na tathmini.

## 2.15 Swali la 15: Ufundishaji wa Mada za Mfano

Katika swali hili, watahiniwa walitakiwa kujadili mambo matano yanayoweza kumfanya mwanafunzi akose usikivu darasani.

Uchambuzi unaonesha kwamba watahiniwa 4504 sawa na asilimia 100 walifanya swali hili ambapo asilimia 2.0 walipata alama 0 hadi 5.5, asilimia 57.3 walipata alama 6 hadi 10 na asilimia 40.7 walipata alama 10.5 hadi 15. Hivyo, kiwango cha ufaulu kilikuwa kizuri kwani asilimia 98 walipata alama 6 hadi 15. Kielelezo Na.15.1 kinaoonesha ufaulu wa watahiniwa hao kwa ufupi.




**Kielelezo 15.1:** *Ufaulu wa Watahiniwa Swali la 15*

Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa waliopata alama za juu 6 hadi 15 walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya usikivu darasani. Pia walielewa vyema matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika;

(i) Kelele darasani: Mwanafunzi anaweza kupoteza usikivu darasani kwani kelele hizo hutokana na mwanafunzi kupiga kelele, sauti za magari kutoka nje au mwalimu kuongea kwa kupayuka darasani.

(ii) Kutokuwa na kazi ya kufanya: Kwa kawaida mwanafunzi wa shule ya msingi asipopewa kazi au mazoezi ya kutosha akili yake mara nyingi huwaza kucheza, na akiwa darasani ataanzisha mijadala mbalimbali inayozua kelele.

(iii) Ufundishaji mbovu na mpangilio mbovu wa hatua za somo: Hali hii hutokea kama mwalimu atafundisha bila kutumia zana bora.

(iv) Kuwepo kwa hali ya upendeleo wakati wa kufundisha: Mwalimu anaweza kuegemea upande fulani wa wanafunzi, mfano kuchagua watu kwa kuwarudiarudia.

Majibu haya yanaonesha kuwa watahiniwa walikuwa na maarifa juu ya *Ufundishaji wa Mada za Mfano* hasa mambo yanayoweza kumfanya mwanafunzi akose usikivu darasani. Kielelezo Na. 15.2 ni sampuli ya jibu sahihi kutoka kwa mtahiniwa mmojawapo.

**Kielelezo Na. 15.2**


15. Mambo yanayoweza kumfanya mwanafunzi akose usikivu darasani.

Usikivu; Ni hali ya kuwa makini kwa kufuata maelekezo yanayotolewa kwa ufasaha. Mwanafunzi upaswa kuwa msikivu darasani ili kuelewa vizuri kile kinachofundishwa. Mambo yanayoweza kumfanya mwanafunzi akose usikivu darasani ni pamoja na:-

Maradhi; Mwanafunzi anapopatwa na ugonjwa akiwa darasani, humfanya kukosa usikivu. Mfano maumivu ya kichwa, tumbo, jino huweza kumfanya kukosa usikivu darasani.

Msongo wa mawazo; Pia mwanafunzi mwenye msongo wa mawazo, ukosa usikivu darasani. Mfano mwanafunzi aliyepata taarifa za msiba wa wazazi, ndugu au rafiki yake mpendwa, umsababisha akose usikivu darasani.

Mavazi ya mwalimu; Mwanafunzi huweza kukosa usikivu kwa sababu ya mavazi ya mwalimu. Mfano nguo zenye mabango au maandishi huwafanya wanafunzi kupoteza muda wa kusikiliza kwa makini wanachofundishwa badala yake husoma maandishi hayo. Au nguo fupi zinazovaliwa na walimu wa kike.


Lugha inayotumika darasani; endapo mwalimu akitumia lugha ya ukali na vitisho huweza kuwafanya wanafunzi kukosa usikivu
Mfano kuwatukana wanafunzi.

Katika Kielelezo Na. 15.2 mtahiniwa aliweza kujadili kwa usahihi mambo matano yanayoweza kumfanya mwanafunzi akose usikivu darasani; aliandika; Lugha, mavazi ya mwalimu, msongo wa mawazo na maradhi.

Kwa upande mwingine, asilimia 2 ya watahiniwa walishindwa kuelewa matakwa ya swali, hivyo kuandika majibu tofuti na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmojawapo aliandika;

(i) Kutokuwa na uvumilivu: Mwanafunzi kukosa uvumilivu darasani wakati wa kusikiliza habari.

(ii) Kuwepo kwa vikwazo mbalimbali: Hii inaweza kumsababishia mwanafunzi kukosa usikivu kwa mfano msamiati mgumu.


(iii) Kutoungana kifikra: Hapa ni baina ya msomaji wa habari na msikilizaji.

(iv) Ukosefu wa uhuru: Vile vile mwanafunzi anapokosa uhuru anaweza kukosa usikivu wake kwa mfano katika uhuru wa usomaji.

(v) Kukosekana kwa hali ya utulivu pia ni sababu mojawapo inayoweza kumfanya mwanafunzi akose usikivu darasani wakati anasikiliza habari inayosomwa.

Majibu haya yanaonesha kuwa mtahiniwa hakuelewa mada ya *Ufundishaji wa Mada za Mfano* hasa kipengele cha usikivu darasani. Kielelezo Na. 15.3 ni sampuli ya jibu la mmoja wa wtahiniwa aliyeandika jibu lisilo sahihi.

**Kielelezo Na. 15.3**


15 Usikivu ni hali ya unyenyekevu na utayari wa kusikiliza jambo kutoka kwa msemaji. Yafuatayo ni mambo matano yanayoweza kumfanya mwanafunzi akose usikivu darasani;

· Mwalimu kushindwa kueleweka kwa wanafunzi pale anapokuwa anafundisha mada kwa wanafunzi hali itakayopelekea kuzua minong'ono kwa baadhi ya wanafunzi kujadili kile anachokifundisha na kupelekea usikivu kutoweka darasani.

· Wanafunzi kukosa kazi ya kufanya darasani itakayomfanya muda wote awe anangaisha kichwa juu ya swali/zoezi lililotolewa ili aweze kulifanya na kulikamilisha kwa wakati.

Walimu kutoingia katika vipindi vyao kwa wakati/pengine asiingie hali inayowapeleke wanafunzi/mwa-

15. nafunzi kukosa utulivu na usikivu na kumfanya aanze kucheza na wenzake na pengine kuwafanya watoke nje ya darasa na kuanza kucheza.

Kiongozi wa darasa kushindwa kuyatumia mamlaka yake vizuri pale mwalimu anapokuwa hayumo darasani na kuwafanya wanafunzi/mwanafunzi akose usikivu darasani hali inayopelekea vurugu kwa wanafunzi wake.

Baadhi ya walimu kushindwa kusimamia mamlaka yao ipasavyo kuanzia kwa mkuu wa shule, mtaaluma, mwalimu wa darasa na mwalimu wa zamu husika katika kusimamia na kuhimiza masuala ya taaluma kwa wanafunzi na kuwahimiza walimu katika majukumu yao hasa Mkuu wa shule na Mtaaluma hali inayowafanya wanafunzi wakose usikivu darasani.


Hivyo basi, hayo ndio mambo yanayoweza kumfanya mwanafunzi akose usikivu darasani ikiwemo mazingira magumu ya ufundishaji na ujifunzaji mfano ukosefu wa vitabu vya kutosha na madawati ya kukalia.

Katika Kielelezo Na. 15.3 mtahiniwa aliandika, mwalimu kushindwa kueleweka, kiongozi wa darasa kushindwa kutumia madaraka yake na baadhi ya walimu kushindwa kusimamia mamlaka yao; badala ya kuandika; kelele, haiba ya mwalimu, njaa, mpangilio wa darasa matumizi ya zana yasiyo sahihi.

## 2.16 Swali la 16: Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la TEHAMA

Katika swali hili watahiniwa walitakiwa kuchambua misingi mitano anayotakiwa kuzingatia mwalimu wa somo la TEHAMA katika kubuni na kutengeneza zana.

Uchambuzi uliofanyika unaonesha kuwa watahiniwa 4376 sawa na asilimia 100 walifanya swali hili, ambapo asilimia 47.2 walipata alama 10.5 hadi 15, asilimia 38.1 walipata alama 6.0 hadi 10.0 na asilimia 14.7 walipata alama 0 hadi 5.5. Ufaulu wa jumla ulikuwa mzuri kwani asilimia 85.3 walipata zaidi ya alama 5.5, kama ilivyooneshwa katika Kielelezo Na. 16.1.




**Kielelezo Na. 16.1:** *Ufaulu wa Watahiniwa Swali la 16*

Uchambuzi wa majibu ya swali hili unaonesha kuwa watahiniwa waliofanya vizuri walikuwa na maarifa ya kuchambua misingi anayotakiwa kuzingatia mwalimu wa somo la TEHAMA katika kubuni na kutengeneza zana. Watahiniwa hawa walielewa swali na walizingatia vema matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mojawapo aliandika kama ifuatavyo:

(i) Kujua idadi ya walengwa: Mwalimu wa somo la TEHAMA anapobuni na kutengeneza zana anatakiwa azingatie idadi ya walengwa ili kila mlengwa aweze kufanikisha kujifunza.

(ii) Ukubwa na ubora wa zana: Mwalimu wa somo la TEHAMA anatakiwa azingatie ukubwa unaofaa wa zana na ubora pia.

(iii) Msingi wa kuzingatia umri na uelewa wa walengwa: Kila zana huendana na umri pamoja na uelewa wa walengwa Kwa mfano ni vigumu kutumia zana ya darasa la saba kwa darasa la tatu.


(iv) Msingi wa kuzingatia lengo mahususi la somo: Kubuni na kutengeneza zana yoyote inatakiwa kujua ni lengo gani linatakiwa lifikiwe.

(v) Msingi unaozingatia upatikanaji wa makunzi ya kutengenezea zana husika.

Majibu haya yanadhihirisha kuwa watahiniwa walikuwa na maarifa na umahiri wa kutosha juu ya uchambuzi wa misingi anayotakiwa kuzingatia mwalimu wa somo la TEHAMA katika kubuni na kutengeneza zana. Kielelezo Na. 16.2 ni mfano wa jibu la mmoja wa watahiniwa aliyejibu kwa usahihi swali hili.

**Kielelezo Na. 16.2**

16 Misingi anayotakiwa kuzingatia mwalimu wa somo la TEHA-
MA katika kubuni na kutengeneza zana.
Zana ni kitu chochote anachokitumia
mwalimu katika kufundihisha na kujifunzia kwa lengo
la kufikisha ujumbe kwa wanafunzi wake, kuna
njia ambazo mwalimu wa somo la tehama anazitumia
kwa ajili ya kutakikisha zana yake inapendeza mfano
kutengeneza, kununua, kuboragua na kuchoro, ifuatayo
ni misingi ya kuzingatia kwa mwalimu wa somo la TEHAMA
katika kubuni na kutengenezo zana ambayo ni:
Kuelewa lengo la somo. Mwalimu unapo
andaa zana zingatia lengo, kwani lengo hilo
litakusaidia wewe uweze kuandaa zana
inayoendana na wanafunzi au mada unayotaka
kufundisha, hivyo ni kuzingatia lengo la mada.
Kuzingatia umri na kiwango cha
uelewa wa mwanafunzi. Mwalimu unapoandaa
zana zako kwa kubuni na kutengeneza inabidi
uzingatie umri na kiwango cha uelewa wa mlengwa
unayetaka kwenda kumfundisha, hivyo basi -
umri na uelewa wa mwanafunzi ni muhimu sana




kuandaa michoro na Vipimo vya zana.
Unapotaka kuandaa zana yako unayotaka kutumia
kufundishia inabidi uandae michoro na vipimo
vya zana yako ambavyo vitakusaidia katika
kutengeneza zana yako kwa ufasaha.
Zingatia uhusiano wa zana na mada
Unatakiwa kuangalia kwanza kuwa zana unayo-
iandaa inaendana na mada unayotaka kufunda
kufundisha na kama haiendani inabidi uandae
upya ili kusudi usije ukawadanganya wanafunzi

Katika Kielelezo Na. 16.2 mtahiniwa alichambua kwa usahihi misingi mitano anayotakiwa kuzingatia mwalimu wa somo la TEHAMA katika kubuni na kutengeneza zana, ambayo ni, kuelewa lengo la somo, kuzingatia umri, vipimo vya zana na uwiano wa mada na zana.

Kwa upande mwingine, watahiniwa ambao walipata alama za chini ya wastani (0 hadi 5.5) hawakuwa na maarifa juu ya misingi mitano anayotakiwa kuzingatia mwalimu wa somo la TEHAMA katika kubuni na kutengeneza zana. Kwa mfano, mtahiniwa mmojawapo aliandika; "Msingi unaozingatia uhusiano kati ya moduli ya TEHAMA na moduli nyingine; Pia, mwalimu anapobuni zana azingatie uhusiano uliopo kati ya zana zinazotumika katika somo la TEHAMA na katika somo jingine''. Pia mtahiniwa mwingine aliandika “Msingi unaozingatia utafutaji, uchambuzi na uwasilishaji”.

Majibu haya yanaonesha kuwa watahiniwa walikosa maarifa kuhusu *Maandalizi ya Ufundishaji* wa somo la TEHAMA hasa katika kipengele cha zana za kufundishia. Kielelezo Na. 16.3 ni mfano wa jibu la mmoja wa watahiniwa aliyeandika jibu lisilo sahihi katika swali hili.

**Kielelezo Na. 16.3**



TEHAMA, Ni somo linalohusu Teknolojia ya
Habari na Mawasiliano, kutokana na kukua kwa
sayansi na teknolojia kumewezesha kuwepo kwa maendeleo
kutokana na kuwepo kwa vifaa vya kisasa vya kufanya mawasiliano
kama vile simu. Ifuatayo ni Misingi inayotakiwa kuzinga
tiwa na Mwalimu wa Somo la TEHAMA katika kubuni na kutengeneza zana

Msingi unaozingatia usalama wa wanafunzi na vifaa, katika ufundishaji wa somo la Tehama ni lazima mwalimu azingatie msingi wa usalama wa wanafunzi na vifaa ikiwa na maana ya kuvitunza vifaa vya tehama visiharibiwe lakini pia wanafunzi wasipate madhara yeyote.

Msingi unaozingatia udadisi na ufikirishwaji wa maarifa, pia katika ufundishaji wa somo la Tehama ni lazima kwa mwalimu kuzingatia msingi huu ili mwanafunzi aweze kuwa mdadisi katika kujifunza mambo mbalimbali.

Msingi unaozingatia kufanya utafiti na uwasilishwaji wa tafiti, pia katika somo la Tehama mwanafunzi anatakiwa kuwa mtafiti na kuwa na uwezo wa kuwasilisha tafiti mbalimbali ambazo zimefanyika.

Msingi unaozingatia usawa wa kijinsia na mtambuko, pia katika kubuni na kutengeneza zana mwalimu anapaswa kuzingatia masuala ya usawa wa kijinsia jambo ambalo halitaleta ubaguzi kwa wanafunzi wa jinsia moja na nyingne

Msingi unaozingatia matumizi ya vitendo, katika kubuni na kutengeneza zana unapaswa kuzingatia matumizi ya vitendo ili mwanafunzi aweze kupata ujuzi mbalimbali na kuweza kuthibitisha baadhi ya mambo.

Hitimisho, katika ufundishaji wa somo la Tehama mwalimu anatakiwa kubuni na kutengeneza zana mbalimbali kwa ajili ya kufundishia, na kujifunzia ili mwanafunzi apende somo zaidi

Katika Kielelezo Na.16.3 mtahiniwa alishindwa kuchambua misingi mitano anayotakiwa kuzingatia mwalimu wa somo la TEHAMA katika kubuni na kutengeneza zana. Mtahiniwa huyu aliandika; misingi inayozingatia vitendo, udadisi, usalama na usawa wa kijinsia.

## 3.0 UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA KILA MADA

Uchambuzi wa majibu haya ya watahiniwa uliofanywa unaonesha kuwa katika somo la TEHAMA maswali yaliandaliwa kutoka kwenye mada zote nne, ambazo ni; *Misingi ya Ufundishaji Somo la TEHAMA*, *Ufundishaji wa Mada za Mfano*, *Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji somo la TEHAMA* na *Upimaji*.

Aidha, maswali 8 yalitoka kwenye mada ya *Ufundishaji wa Mada za Mfano*, 2 yalitoka kwenye mada ya *Misingi ya Ufundishaji* na *Ujifunzaji Somo la TEHAMA*, 3 yalitoka kwenye mada ya *Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji Somo la* TEHAMA 3 yalitoka kwenye mada ya *Upimaji*. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, mada zote zilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu. Hata hivyo, mada ya *Ufundishaji wa Mada za Mfano* ilikuwa na ufaulu zaidi ya (80.8%), ikifuatiwa na *Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji Somo la TEHAMA* (77.7%). Aidha, mada ya *Upimaji* ilikuwa na ufaulu wa asilimia 74.4, huku mada ya *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji Somo la TEHAMA* ikiwa ya mwisho katika ufaulu kwa kuwa na asilimia 69.5 (Rejea kiambatisho).

## 4.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 4.1 Hitimisho

Kwa ujumla somo la TEHAMA lilikuwa na ufaulu mzuri (99.78%). Uchambuzi unaonesha kuwa mada zote zilizokuwa kwenye muhtasari wa daraja la IIIA ambazo ni *Misingi ya Ufundishaji Somo la TEHAMA*, *Ufundishaji wa Mada za Mfano, Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji somo la TEHAMA na Upimaji* zilifanyiwa upimaji.

Kwa ujumla mada zote zilifanyika vizuri isipokuwa mada ya *Upimaji* kipengele cha utunzi wa maswali ya kuchagua, *Ufundishaji wa Mada za Mfano* kipengele cha mbinu za kufundishia, *Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji Somo la TEHAMA*, hususani kwenye vipengele vya huduma za posta na usikivu.

### 4.2 Mapendekezo

**Wanafunzi au Watahiniwa**

(a) Watahiniwa wanashauriwa kuzingatia maelekezo wanayopewa na walezi wao hasa katika kujifunza.

(b) Watumie teknolojia inayowazunguka kujipatia maarifa mbalimbali ya husuyo TEHAMA na maisha ya kila siku kwa ujumla.
(c) Wawapo kwenye vyumba vyao vya mitihani wahakikishe wanasoma na kuelewa kwa ufasaha matakwa ya swali na kujibu kulingana na matakwa hayo.

**Wakufunzi**

(a) Wafundishe na kukamilisha mada zote za somo la TEHAMA kwa ufanisi.
(b) Wawaelekeze watahiniwa kwa kina namna ya kujibu aina mbalimbali za maswali.
(c) Wakati wa kufundisha *Mada za Mfano* hasa kipengele cha mbinu za kufundishia wakufunzi wahakikishe wanawafundisha aina mbalimbali za mbinu hizo na kuwaeleza namna ya kuzitumia.

**Watunga sera**

(a) Mabadiliko ya mitaala yaendane na madadiliko ya miundo mbinu ya mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.
(b) Uimarishaji wa mafunzo kazini uzingatiwe hasa kila kunapotokea mabadiliko ya mitaala.

**KIAMBATISHO**

**Ufaulu wa Watahiniwa kwa kila Mada**

| Na | Mada | Namba ya Swali | % ya watahiniwa waliopata 40% ya jumla ya alama ya swali au zaidi | Wastani wa Ufaulu | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ufundishaji wa Mada za Mfano | 3 | 78.4 | 80.8 | Vizuri |
| | | 4 | 96.6 | | |
| | | 6 | 91.1 | | |
| | | 7 | 54.6 | | |
| | | 8 | 39.7 | | |
| | | 12 | 90.6 | | |
| | | 13 | 97.7 | | |
| | | 15 | 98 | | |
| 2 | Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la TEHAMA | 5 | 53.9 | 77.7 | Vizuri |
| | | 10 | 94 | | |
| | | 16 | 85.3 | | |
| 3 | Upimaji | 2 | 32.7 | 74.4 | Vizuri |
| | | 9 | 94 | | |
| | | 14 | 96.5 | | |
| 4 | Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji Somo la TEHAMA | 1 | 41.3 | 69.5 | Vizuri |
| | | 11 | 97.6 | | |

cmyk